Nipashe
Jumatatu Februari 15, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580492
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



MAKALA MAALUM

**Kibano** kikali kinavyowanyatia maofisa ugani

UKURASA 4



**Bashiru** ataka sheria kali kwa wanaodhalilisha wanawake

UKURASA 8

**Messi aifikia rekodi ya Xavi Barcelona**

UKURASA 20



# HESLB yampa deni asiye mnufaika

• **Ni** mtumishi aliyeandikiwa mil. 18/-... *Endelea Ukurasa 2*



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na uongozi wa Wilaya ya Temeke katika eneo la Kijichi Mbagala wakati wa ziara yake ya siku mbili ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani Dar es Salaam, jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

## Mvua ya mawe nusu saa yaacha vilio, hasara

UKURASA 3







Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## Agizo la JPM larejesha vizimba kwa saa mbili

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAREJEA NA UJUMBE MZITO CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# HESLB yamwandikia deni la mil. 18/- mtumishi asiye mnufaika

**Na Thobias Mwanakatwe**

MTUMISHI wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Wilaya ya Biharamuro mkoani Kagera, Eladi Lugayelukamu, ameilalamikia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kwa kumwandikia deni la Sh. milioni 18 na kuanza kumkata katika mshahara wake wakati hajawahi kuomba mkopo.

Mtumishi huyo aliwasilisha malalamiko hayo kwenye kipindi cha Papo kwa Papo kinachorushwa na runinga ya Channel Ten ambacho kinaendeshwa kila Jumamosi na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole.

Alisema HESLB imekuwa ikimkata kiasi cha shilingi 81,900 katika mshahara kila mwezi kwa muda wa miezi saba wakati hajawahi kuomba mkopo katika bodi hiyo wala kusoma katika chuo kikuu chochote nchini na nje.

Lugeyelukama alisema baada ya kubaini kukatwa kiasi hicho, aliwasilisha malalamiko yake na nyaraka kwa wahusika ambapo ilipofika Machi 2018 Bodi ilisitisha kumkata mkopo huo.

Aliongeza kuwa katika hali ya kushangaza tangu mwaka 2018, alipoomba arejeshewe fedha ambazo alikatwa kimakosa, amekuwa akipata usumbufu na kwamba hadi sasa hajarejeshewa.

Kufuatia malalamiko hayo, Polepole alimpigia simu Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, kupata ufafanuzi wa jambo hilo.

Badru alisema kiutaratibu kama mtumishi huyo alikuwa akikatwa fedha wakati sio mnufaika wa mikopo huyo, inatakiwa asimamishiwe na kwa kuwa suala hilo lilishafanyika bodi yake itafuatilia haraka ili aweze kurejeshewa fedha zake.

Naye Polepole alimtaka mtumishi huyo atakapolipwa fedha hizo atoe mrejesho, na kwamba serikali ya CCM itahakikisha inafuatilia suala hilo ili haki ipatikane.




Diwani wa Kata Ijumbi, Wilbad Kakuru, akionesha majengo yaliojengwa na mdau wa maendeleo, Prosper Rweyendera na kuyakabidhi kwa Serikali ya Kijiji hicho kwa muda mrefu bila kufanyiwa kazi, ikiwamo huduma ya afya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kifusi kilivyoua wachimbaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wa wadogo wawili katika mgodi wa Mwime uliopo Kata ya Zongomeala, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamekufa baada ya kuangukiwa na kifusi cha udongo.

Ajali hiyo ilitokea wakati wakiendelea na shughuli za uchimbaji wa madini.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, ACP Deobora Magiligimba, amethibitisha kutokea kwa vifo hivyo, na kueleza kuwa tukio hilo lilitokea Ijumaa majira ya asubuhi katika duara namba 11C mgodini hapo.

Magiligimba aliwataja waliokufa ni Kija Walaga (25), mkazi wa Kijiji cha Mwime Kata ya Zongomela na Msonga Giti(36), mkazi wa Ilima mkoani Simiyu.

Magiligimba alisema chanzo cha ajali hiyo ni wachimbaji hao kuendelea na shughuli za uchimbaji bila kuchukua tahadhari kwani shimo hilo lilikuwa halitumiki kwa muda mrefu kwa sababu ya matengenezo.

Alisema milii imehifadhiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ikisubili ndugu kwa ajili ya taaratibu za mazishi. Magiligimba aliwataka wachimbaji wadogo kufuata miongozo ya iliyowekwa na viongozi wao na kamati za madini juu ya uchimbaji salama katika maeneo yao kuepukana na ajili za uzembe.

Mmoja wa wachimbaji wadogo ambae hakutaka jina lake kutajwa gazetini, alisema duara hilo lilikuwa lina muda mrefu tangu kusimamisha uzalishaji kwa ajili ya kusubili matengenezo ya kufunga magogo(matimba) shimoni, lakini walishangaa kuona watu wanaendela na shughuli za ushimbaji mpaka ilipotokea ajali hiyo.


The ILO Country Office for Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda and Burundi.

SALE OF USED VEHICLE

The Office invite bids for purchase of one (1) used vehicle on "as is where is" basis as per details below.

**Car make:** Toyota
**Model:** Land cruiser
**Body type:** Station wagon
**Color:** White
**Engine capacity:** 4500 cc
**Fuel type:** Diesel
**Seating capacity:** 9
**Year of manufacture:** 2008

For the interested bidders, send your bid via email **darprocurement@ilo.org** not later than 16:00 hrs, Friday 19 February 2021.

The successful bidder will have to deposit full payment to the office bank account within 3 days.

For those who would like to see the vehicle, Please send email through **darprocurement@ilo.org** , a reply will be sent to notify the date and time for your visit at the Office premises, (Maktaba street, Kazi House, Plot no. 76/27 & 105/27), before the closure of submitting bids (19/02/2021).


## Saa 2 zarejesha vizimba agizo la JPM

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

AGIZO la Rais John Magufuli la kuwataka watumishi wa serikali kurudisha vibanda walivyojimilikisha katika soko Kuu la Chief Kingalu mkoani Morogoro, limeanza kutekelezwa.

Tayari watumishi 16 wa Manispaa hiyo ya Morogoro wamerudisha maeneo waliyokuwa wamejimilikisha na waliyokuwa wamewakodishia wafanyabiashara katika soko hilo.

Akizungumza wakati wa kuendesha uhakiki wa maeneo katika soko hilo uliofanywa na kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo kwa kushirikiana na menejimenti ya halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, alisema watumishi hao walitumia msaa mbili tu kurejesha vibanda hivyo badala ya saa saba walizokuwa wamepewa.

"Tuliitisha mkutano na watumishi wote wa Manispaa na kuwapa saa saba wawe wamesalimisha maeneo na kurudisha fedha walizochukua, ndani ya saa mbili hadi tatu, watumishi 16 walijisalimisha na kurudisha maeneo hayo kwa maandishi," alisema Msulwa.

Msulwa alisema agizo jingine ambalo wametekeleza ambalo walipewa na Rais Magufuli ni kuhakikisha watumishi waliokuwa wamewapangisha wafanyabiashara katika soko hilo akiwamo Aika Massawe wanarejesha mara moja fedha walizokuwa wakichukua katika pango.

Pia, alisema tayari wamerekebisha kasoro mbalimbali zilizokuwa katika soko hilo ikiwamo mfumo wa uongozi, kufanya uhakiki kwa wafanyabiashara wa zamani na waliojilimbikizia maeneo.

Alisema wafanyabiashara wa zamani watapatiwa maeneo na wale waliokuwa wamejilimbikizia watayarejesha ili yagawiwe kwa wanaostahili.

"Wafanyabiashara 430 wamehakikiwa, tumebaini wengine wana maeneo zaidi ya moja, walifanya ujanjaujanja kujimilikisha maeneo ya watu hata ya waliofariki," alisema Msulwa.

Alisema vipo vioski 70 na vizimba 30 ambavyo viko wazi na kwamba vitajazwa ndani ya siku mbili.

Pia, alisema bado wanafanya uhakiki wa kutambua watumishi wengine wenye vibanda katika soko hilo ambao wanatumia majina ya watu wengine, na kwamba watakaowabainika watanyang`anywa na kuvigawa kwa wafanyabiashara wanaostahili.

Pia alisema watapitia upya mchakato wa awali uliotumika kupanga gharama za umiliki wa vibanda katika soko hilo.

HABARI KITAIFA

# Mvua ya mawe yaleta madhara

Na Salome Kitomari

MVUA ya Mawe imesababisha madhara kwa kuharibu mazao na miundombinu katika baadhi ya maeneo ya kata za Ilongero na Mudida, Wilaya ya Singida mkoani Singida.

Mvua hiyo iliyonyesha kwa nyakati tofauti ilinyesha kwa nusu saa Kata ya Ilongero, ikiwa na madhara makubwa kwenye mazao aina ya mahindi, lakini hadi sasa hakuna madhara kwa binadamu na makazi yao.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskasi Muragili, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alithibitisha kuwapo kwa maafa hayo katika kata hizo, na kwamba wataalamu wapo kwenye vitongoji vilivyoathiriwa kwa ajili ya kufanya tathmini.

Aidha, Diwani wa Kata ya Ilongero, Issa Mwiru (CCM), aliiambia Nipashe kuwa mawasiliano ya kata yake na Kata ya Mlama kutokana na kipande cha barabara kuzolewa na maji.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, katika Kata ya Ilongero mvua ilinyesha Jumamosi majira ya saa 10 jioni na ilikuwa ya nusu saa, lakini ilikuwa ya mawe na madhara makubwa ni kwenye mazao ya mahindi.

"Mvua kubwa imeleta madhara, mvua ya mawe imesababisha matawi ya mahindi kuchanwa chanwa na kubaki mashina," alisema na kuongeza:

"Timu ya wataalamu inafanya tathmini ili kujua madhara kiasi gani. Kwa taarifa za awali ni kuwa mahindi yalikuwa machanga, ila hakuna madhara mengine."

Aidha, alisema baada ya tathmini wataalamu watajua idadi ya ekari zilizoathiriwa na kwamba leo watatoa taarifa ya hali ya uharibifu.

"Hadi sasa hakuna uharibifu wa miundombinu, ila kwa mvua zilizokuwa zinaendelea. Mvua kama hii haijawahi kunyesha, imejirudia baada ya siku za hivi karibuni kunyesha Kata ya Mudida na kuathiri vijiji vitatu," alisema.

Kwa mujibu wa Muragili, tathmini ya aliwa inaonyesha kuwa mazao yalikuwa machanga na yataeza kuchepua tena na kwa ambao yalifikia kwenye mbelewele wameshauriwa kupanda alizeti ili wauze na kupata chakula baadaye.

"Kata ya Mudida mahindi yalikuwa madogo yanaweza kuchepua na kuendelea na tunafuatilia yako vizuri. Wananchi 13 waliathirika mazao yao yalifikia hatua ya kuchaua yaliharibia kabisa hayawezi kuota, tumewashauri wapande alizeti ili aweze kununua chakula,"alisema.

### DIWANI ASIMULIA

Diwani wa Kata ya Ilongero, Issa Mwiru (CCM), alisema madhara iko kwenye mahindi katika vijiji vya Ilongero, Madagha, Mhango, Itamka na Mlama ambako mahindi yamechanwa na kubaki mashina yamesimama ambayo yalikuwa yameshafikia kutoa mbelewele.

### MVUA YA MAWE NI NINI

Joyce Makwata, ni mchambuzi wa hali ya hewa wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), alisema mvua za mawe hutokana na mawingu mazito ya radi yanayotokana na vipande vya barafu na matone ya maji, vipande vikiwa katika wingu vinaendelea kukua, wingu inashindwa kuhimili uzito na ndipo vinaanguka na kuitwa mvua ya mawe.

"Hali ya anga ikiwa ni joto vinayeyuka na kushuka ardhini kama mvua, lakini kukiwa na joto kali ndiyo vinayeyuka tunapata mvua, joto la kawadi vinakuwa kwenye hali ya ugumu na kuitwa mvua ya mawe,"alifafanua.

Makwata anasema mvua hiyo hutokea maeneo ya tropikali na kwenye miinuko ndiyo huweza kushuka mawe kulingana na hali ya joto angani na maeneo mengine ya ukanda wa Pwani hunyesha kama mvua ya maji.

## Samia awaonya wauza maji binafsi

Na Beatrice Shayo

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewaonya wafanyabiasha wanaouza maji ya visima kwa wananchi Kigamboni kutafuta biashara nyingine ya kufanya na siyo kuichafua Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA) kuwa inauza maji bei ghali.

Akikagua mradi wa maji wa Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya kutatua kero za wananchi ya huduma hizo, alisema kumekuwa na usambazaji wa taarifa kuwa maji ya DAWASA ni ghali jambo ambalo siyo kweli.

"Niwaombe sana wauza maji wa Kigamboni wasituchafulie wala msibeze juhudi zilizowekwa na serikali kuleta maji kwa wananchi kwa sababu tu ya biashara yenu ya maji," alisema.

"Maendeleo ni kubomoa na kujenga umekosa biashara ya maji tafuta biashara nyingine umeshapata fedha ya kutosha kwenye maji wekeza katika biashara nyingine lakini usituchafulie," alisema.

Aidha, alisema mradi huo wenye visima 12 umetumia Sh. bilioni 23 na kwamba zitazalishwa lita milioni 15 na kila uniti itauzwa kwa Sh.1,600.

"Uniti moja iliyogharimu mabilioni ya fedha itauzwa kwa Sh. 1,600 bado anasimama mtu anasema maji ya DAWASA yanauzwa gharama kubwa msinunue kwa sababu tu amechimba visima anazalisha maji ya chumvi na kuwauzia maji ya chumvi hii siyo sawa wana Kigamboni maji ya DAWASA ni salama," alifafanua.



Mkuu wa Kiwanda cha Kutengeneza Chanjo cha Hester, Dkt. Umapati Dasgupta (kulia), akimueleza jambo Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (kushoto), alipotembelea kukagua kiwanda hicho kilichopo wilayani Kibaha, Mkoani Pwani. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

## Waziri anusa ufisadi kituo cha afya

Na Nebart Msokwa, MBEYA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Festo Ndugange, amenusa ufisadi katika Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka kilichopo jijini Mbeya huku miundombinu yake ikiwa imechakaa.

Akizungumza juzi baada ya kukagua kituo hicho, alisema alipohoji kuhusu idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa kwenye kituo hicho kwa siku na mapato yanayokusanywa haviendani hata kidogo na hivyo akadai kuwa kuna sehemu mapato hayo yanavuja.

Alisema kuwa alielezwa na Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. Stella Moses, kuwa kwa siku wanawahudumia watu 300 ambao kati yao 100 wanatibiwa kwa bima na 200 wanalipia huduma ikiwemo Sh. 3000 za kujiandikisha.

Alisema kwenye taarifa ya mapato ya Kituo hicho alielezwa kwa siku wanakusanya Sh. 300,000 pekee, kiwango ambacho alisema hakiendani kabisa na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa kituoni hapo na kwamba wanatakiwa kuziba mianya yote ya upotevu wa mapato.

Dk. Ndugange alisema kituo hicho kina uwezo wa kukusanya zaidi ya mara tatu ya mapato ambayo yanakusanywa kwa sasa, na kwamba kama wagonjwa wote 200 wanaohudumiwa wanalipa Sh. 3000 za usajili ilitakiwa zipatikane Sh. 600,000 lakini wao wanakusanya nusu.

Alisema wanashindwa kufikia malengo kwa sababu ya ubadhrifu na hivyo akawataka kuboresha mfumo wa ukusanyaji na kuweka mifumo mizuri ya matumizi.

Aidha alibaini kuwa hakuna utaratibu mzuri wa uingizwaji wa dawa kwenye kituo hicho kutoka serikalini na namna ambavyo zinatoka kwa maelezo kuwa alipohoji kuhusu uwapo wa taarifa za utokaji na uingiaji wa dawa hizo mwezi huu hakupatiwa.

## MAKALA MAALUM

# Mfumo kuwapa kibano maofisa ugani

- Sasa kufuatiliwa kwa mfumo wa GPS kila siku
- Upimaji wa udongo kuwa bure kwa wakulima
- Uhaba wa mafuta ya kula kuwa historia nchini

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KILIO cha wakulima nchini kutowaona maofisa ugani shambani kimepata majibu, baada ya serikali kutangaza kuanza kuwafuatilia kila siku watumishi wake hao kwa kutumia kifaa maalum cha kukokotoa mawasiliano ya kijiografia (GPS).

Maofisa ugani hao ni watakaokuwa wanatumia pikipiki 7,000 ambazo zitagawanywa katika halmashauri zote za wilaya msimu ujao.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alibainisha mpango huo alipokuwa anatolea ufafanuzi hoja mbalimbali za wabunge zilizoelekezwa kwenye wizara hiyo wakati wa mjadala bungeni juzi.

"Tumeanzisha ile call centre (kituo cha ufuatiliaji) hapa wizarani, ambayo GPS itatumika kujua kama ofisa ugani anafanya kazi katika eneo lake.

"Tutawapatia Ipad (kishikwambi) ambacho watakuwa wanajaza taarifa kwenye call sheet (fomu maalum za simu) za kila siku kuonyesha shamba gani amelitembelea na amemtembelea mkulima gani.

"Hatua ya pili katika hizi agricultural centres (vituo vya kilimo) tutakazoweka katika kila wilaya, tutagawa pikipiki 7,000 kwa maofisa ugani wa nchi nzima katika msimu ujao na kila pikipiki tutaifunga GPS," Bashe alisema.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe. **PICHA: MTANDAO**

### KUPIMA UDONGO BILA MALIPO

Bashe pia alizungumzia upimaji wa afya ya udongo, akisema wizara inakuja na mpango maalum katika bajeti ijayo, ambao unaelekeza uanzishaji wa vituo vya kilimo katika kila halmashauri nchini.

Alisema utekelezaji wa mpango huo utakwenda sambamba na ugawaji wa vifaa vya maabara ya kisasa inayotembea.

"Lab equipment (vifaa vya maabara) ambavyo ni mobile equipment (maabara ya kisasa inayotembea) zitatumika kupima na kutoa huduma ya afya ya udongo kwa wakulima bure ili kila mkulima aweze kupimiwa kipande chake cha ardhi.

"Na hii ni teknolojia rahisi, kama wizara tumeamua kuchukua hatua kwa sababu mkulima kupima afya ya udongo kwa kila sampuli inamgharimu kiasi cha Sh. 40,000 mpaka 100,000 kutokana na umbali wa eneo ambalo maabara anapimia," alisema.

Ili kuwa na kilimo chenye tija, Bashe alisema wizara hiyo itatumia teknolojia rahisi ya vifaa vya maabara ambavyo vitatumika kufanya upimaji wa ubora wa udongo na kuanisha aina za udongo.

Baada ya hapo, mkulima atapatiwa hati ya kumwonyesha kwamba udongo wake una sifa zipi na unafaa kwa zao gani na unatakiwa kutumiwa vipi.

### MFUKO WA UTAFITI

Naibu waziri huyo alisema wanajipanga kuimarisha utafiti na maendeleo ya mbegu na serikali imeamua haitategemea tena fedha za wahisani katika kufanikisha suala hilo.

Alisema serikali imepanga kuanzisha Mfuko wa Utafiti, ambao kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), itatafuta fedha na kuhudumia masuala yote ya utafiti nchini.

"Na kwa kuanza katika bajeti ijayo, tutaleta mpango mkakati tulionao wa kuzalisha tani 5,000 za mbegu OPV za alizeti ili katika msimu ujao wa kilimo tuwagaiwe wakulima na tupate tani 123,000 za mafuta ya alizeti kutokana na mahitaji ya mafuta ya kula nchini kuwa juu," alisema.

Kuhusu pembejeo, Bashe alisema serikali imeamua kubadili mfumo, baada ya kufanya utafiti kwenye pamba na sasa wanajipanga kufanya kwenye korosho msimu ujao.

Vilevile, alisema kwa mwaka huu kwenye pamba, wamewagawia wakulima mbegu na dawa bila malipo na watafanya hivyo hivyo kwenye korosho.

"Tumeshatangaza zabuni ya kugawa dawa za korosho kwa wakulima bure na tutawapatia dawa hizo. Tumefanya kwa Bulk Procurement (ununuzi wa pamoja) na hii itatupunguzia gharama na tunatarajia sulphur safari hii itapungua bei itakayoenda kwa wakulima na tutahuisha gharama kutoka kwenye mjengeko wa bei." alisema.

Kuhusu zao la chai, Bashe alisisitiza kwamba serikali imeamua na imeanza mchakato wa kuweka soko Dar es Salaam, ambalo litakuwa ni kwa ajili ya kuuza zao la chai moja kwa moja.

Alisema Kiwanda cha Chai cha Mponde kilichoko Bumbuli, Wilaya ya Lushoto mkoani Tanga, nacho kitafunguliwa.

"Mwaka huu, tutasafirisha korosho zote kwa kutumia magunia ya katani na nitumie Bunge hili kumwambia mwekezaji ambaye ana viwanda viwili vya magunia cha Morogoro na Kilimanjaro, tunampa kazi, akishindwa tutapeleka mapendekezo serikali kumnyang'anya viwanda hivi tuwape wawekezaji wengine," alisema.

### SHERIA MPYA YAJA

Akijibu hoja za wabunge waliochangia mjadala wa hotuba ya Rais John Magufuli aliyoitoa Novemba 13, mwaka jana alipozindua Bunge la 12, Bashe alisema mabadiliko makubwa yanakuja katika Sekta ya Kilimo nchini kutokana na azma ya serikali kuja na sheria mpya ya kulinda mbegu za asili za mazao ya chakula na biashara.

Bashe alisema sheria hiyo itasaidia mpango wake wa uzalishaji wa mbegu ili kutatua tatizo lililopo nchini.

"Kwa sasa, mahitaji ya lazima ya mbegu nchini ni tani 371,000, lakini mbegu zinazozalishwa za kisasa ni tani 76,000.

"Tani 11,000 ni mbegu ambazo Tanzania inaagiza kutoka nje, na mbegu zinazobaki ni mbegu zetu za asili ambazo tumekuwa tukizitumia katika hatua mbalimbali,' alisema.

Bashe alisema wizara imetenga Sh. bilioni 179 kwa ajili ya uwekezaji wa utafiti na uhaulishaji wa mbegu kwa miaka mitano ijayo.

"Tunachokifanya hivi sasa, tunawekeza katika research (utafiti) kwa ajili ya kuendeleza mbegu aina ya OPV na highbred, lakini wakati huo huo kutunza mbegu zetu za asili.

"Sisi kama Wizara, Mungu akitujalia tunakuja na sheria maalum ya kulinda traditional seeds (kulinda mbegu za asili) ili ziweze kufanyiwa purification (kuchujwa) na ziweze kufanyiwa maendeleo,"alisema.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, mbegu zinazojadiliwa ni nne ambazo ni traditional seeds (mbegu za asili), mbegu za OPV, highbred na teknolojia ya GMO (uhandisi jeni).

"Kama nchi, tumesema hatutumii mbegu za GMO na hatutaruhusu, na tumeweka utaratibu wa wazi kwamba highbred seeds ambayo tunazungumzia, mbegu mbili za kiume na kike zenye sifa mbili tofauti zinazofanyiwa cross breeding (upandikizaji) na hapa msingi wake ni mbegu za asili.

"Unaweza ukakuta mbegu ya asili A, ina sifa ya uzalishaji mkubwa lakini haina uwezo wa ku-resist (kuhimili) magonjwa.

"Wataalamu wetu wanafanya kazi ya kuzipandikiza hizi mbegu mbili ili kupata mbegu ambayo ina sifa zote mbili ili kumsaidia mkulima," alisema.

### MBEGU ZA MAFUTA

Kuhusu uzalishaji wa mbegu za mafuta ya alizeti ili kukabiliana na mfumuko wa bei ya mafuta ya chakula, Bashe alisema wizara imechukua hatua ya kupambana na tatizo la uhaba wa mafuta nchini.

Alisema hivi sasa nchi inahitaji uzalishaji wa tani 5,000 za mbegu za highbred na mbegu za OPV za alizeti ili kufikia uzalishaji unaohitajika wa mbegu za mafuta.

### YATIA SAINI MoU

Kwenye mazao ya chakula na biashara hasa ngano, Bashe alisema serikali imetia saini hati ya makubaliano (MoU) na wanunuzi wa ngano na uchakataji wa ngano ndani ya nchi, baada ya Wizara ya Kilimo kuweka lengo la kuzalisha tani 150,000 msimu ujao.

"Tunatengeneza utaratibu ambao tumekubaliana na sekta binafsi kwamba hatutoagiza ngano kutoka nje, kabla ya kununua ngano ya ndani yote.

"Na katika msimu huu unaokuja, tutagawa jumla ya tani 36,000 za mbegu kwa ajili ya kuzalisha ngano katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

"Hapa Dodoma, kule Wilaya ya Bahi, tumefanya pilot study (utafiti) na imeonekana mbegu ina mature (inamea) kwa muda mfupi kuliko wakati wowote, na Mkoa wa Rukwa tutagawa hizi mbegu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Uhaba wa wataalamu tishio kwa wawekezaji

**Na Mbaraka Kambona,** KIBAHA

MRATIBU na Mkurugenzi wa Opereshen, kiwanda cha kutengeneza chanjo cha Hester, Tina Towo Sokoine, amesema lengo la kiwanda hicho ni kutumia wataalamu wa ndani, lakini uhaba wa wataalam wa masuala ya sayansi wenye ujuzi hasa wa vitendo, unaelekea kukwamisha dhamira yao.

Towo aliyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa kiwanda hicho kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, alipotembelea kiwanda hicho kilichopo wilayani Kibaha, Mkoani Pwani Jumamosi.

Alisema wana wataalamu watatu tu kutoka nje ya nchi, ambao wamewaajiri katika kiwanda hicho, lakini kwa hali ilivyo wanaona watashindwa na labda wanaweza kuomba vibali vingine vya kuajiri wataalamu kutoka nje.

"Nia yetu ni kufanyakazi na Watanzania tu, lakini bado vijana wengi tunaowafanyia usahili wanakosa ujuzi hasa wa vitendo, tunaiomba Serikali na vyuo vinavyoandaa hawa wataalamu kuhakikisha wanajikita katika elimu ya vitendo na sio nadharia peke yake ili kukidhi mahitaji ya sasa na kulinda ajira za Watanzania," alisema Towo.

Kuhusu uzalishaji, Towo alisema wanatarajia kuzalisha chanjo ya kwanza Aprili mwaka huu, huku akiiomba Serikali kuona uwezekano wa taasisi zinazohusika na kusimamia uwekezaji kuunganishwa ziwe na lugha ya pamoja ili kumfanya muwekezaji aweze kupata huduma zote sehemu moja bila kuhangaika kama ilivyosasa.

Naye, Prof. Elisante Ole Gabriel aliutaka uongozi wa kiwanda hicho kuhakikisha wanazalisha chanjo zenye ubora ili nchi iweze kuondokana na utegemezi wa chanjo na bidhaa nyingine za mifugo kutoka nchi za nje.

"Lengo la Wizara ni kuhakikisha kuwa nchi inaondokana na uagizaji wa chanjo kutoka nje, tunatamani kuwa na chanjo tunazoweza kudhibiti ubora wake na tuwe na uhakika nayo, hivyo uwepo wa kiwanda hiki kutatusaidia kuzalisha chanjo hapa hapa nchini ili kukidhi mahitaji ya Wafugaji wetu na Watanzania kwa ujumla," alisema Prof. Ole Gabriel.

Aliongeza kuwa Serikali inaweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili mahitaji ya wafugaji na wananchi yawe yanashughulikiwa ndani ya nchi.

# Katibu Mkuu Kiongozi ataja yanayowakwaza wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, ameutaja mfumo dume na kukosekana utayari miongoni mwa wanawake kujitokeza kwenye uongozi kuwa ni mambo yanayowakwamisha kinamama kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Aliyasema hayo jana huko Kikwajuni, wakati akizindua kitabu cha mwongozo wa ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na siasa, kilichotayarishwa na asasi za kiraia ikiwemo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

Zena alisema katika changamoto hizo zipo ambazo zinahusisha serikali akitaja suala la kutunga sera na sheria na kuzitaka asasi za kisheria kuzipitia sheria zote zinakwamisha juhudi za wanawake kuwa viongozi.

Alisema serikali ya awamu ya nane chini ya Dk.Hussein Ali Mwinyi, imeahidi na kusisitiza kuweka mazingira bora kwa wanawake kufikia malengo ya kisiasa kwa ajili ya kushiriki katika harakati za kisiasa.

Aliongeza kuwa malengo hayo yamefikiwa kwa kuwapo uteuzi wa wanawake katika uongozi kwenye nafasi za mawaziri, makatibu wakuu na wakuu wa mikoa pamoja na wilaya.

"Miongoni mwa kigezo kikubwa cha wanawake kushika nafasi ya uongozi ni elimu.....asasi zinazojikita katika kutoa elimu zisaidie mapambano ya kuwapatia elimu wanawake,"alisema Katibu Mkuu Kiongozi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake (ZAFELA) Jamila Mahmoud, alisema lengo la mradi wa miaka minne wa wanawake na uongozi ni kujenga msingi imara utakaowawezesha kinamama kuyafikia malengo ya uongozi.

Alisema wakati umefika kwa wanawake kugombea nafasi za uongozi katika majimbo ya uchaguzi kwa vile yapo mafanikio kwa baadhi ya wanawake waliofanya hivyo na kufaulu.

"Mradi wa wanawake na uongozi unaofadhiliwa na Norway una lengo la kujenga uwezo kwa wanawake kushika nafasi za uongozi wa kisiasa na kuwa wakilishi kwenye majimbo ya uchaguzi"alisema Jamila.

Mkurugenzi wa TAMWA, Dk. Mzuri Issa, aliitaka jamii kubadilisha mitazamo hasi kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke ili uwe rafiki wa mwanamke ni mwanamke hivyo kuungana pamoja katika kuwapa nafasi kinamama kuwa viongozi.

Akitoa nasaha zake, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Khatib aliwataka wanawake wajitokeze kugombea nafasi za uongozi na wasikate tamaa kwani mazingira ya kushiriki katika siasa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mazuri.

"Wanawake wenzangu nawaomba mjitokeze kugombea katika majimbo ya uchaguzi....hakuna vikwazo vitakavyowakwamisha kutekeleza dhamira hiyo,"alisema Salama.



Washindi wa shindano la Tukutane Ngome Kongwe lililoendeshwa na Benki ya CRDB wakiwa moja ya jengo la Mji Mkongwe 'Stone Town' walipotembelea Zanzibar kufanya utalii wa ndani. Washindi hao pia walipata nafasi ya kuhudhuria tamasha la Sauti za Busara lililofanyika visawani humo wikiendi hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango wa kupima ardhi nchi nzima waja

**Na Munir Shemweta**

KATIKA kuhakikisha ardhi ya Tanzania inapangwa na kupimwa ,Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuja na mkakati wa kuwatumia wapima wa kati (Para Surveyors) na vyuo vyake vya ardhi vya Morogoro na Tabora katika kuharakisha upimaji wa ardhi nchini.

Akijibu hoja za Wabunge juzi katika kikao cha Bunge, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Angeline Mabula, alisema mpaka sasa asilimia 25 tu ya ardhi ya Tanzania imepimwa ikijumuisha viwanja 2,349,626 na mashamba 28,312, huku jumla ya hati 1,559,609 zikiwa zimetolewa.

Alisema, kutokana na Wizara kuwa na watumishi wachache 1400 kati ya 2500 wanaohitajika aliowaeleza kuwa hawezi kukidhi haja katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na kusisitiza kuwa wameona waanze kutumia wapima wa kati pamoja na vyuo vya ardhi kutekeleza azma ya kupima ardhi nchini.

Alisema, Wizara yake ilijaribu kutumia kampuni ya upimaji katika zoezi la upimaji shirikishi, lakini kati ya kampuni 134 ziliyopewa kazi ni kampuni 34 tu ndiyo yaliyofanya vizuri wakati wa utekelezaji zoezi hilo.

"Wizara sasa itaelekeza nguvu katika

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba msibweteke, sasa ifanyieni kazi Al Ahly CAF

**WAWAKILISHI** wa Tanzania na ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, wameanza vizuri hatua ya makundi kwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya AS Vita ya DR Congo.

Simba ambayo mbali na AS Vita katika Kundi lao la A, ipo pamoja na Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan, kwa sasa inaongoza kundi hilo ikiwa na pointi tatu na bao moja wakati huu Wamisri hao wakitarajiwa kuwakaribisha Wasudan kesho katika mechi ya kukamilisha raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Baada ya mechi hiyo, Al Ahly itajiandaa kwa safari ya kuja jijini Dar es Salaam tayari kuwakabili wenyeji wao, Simba katika mechi ya raundi ya pili itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Februari 23, mwaka huu, huku Al- Merrikh ikikaribisha AS Vita nchini Sudan.

Kwa ujumla mechi ya Simba dhidi ya Al Ahly, itakuwa si ya kitoto kwani Waarabu hao wa Misri ndio mabingwa watetezi huku wakitoka kwenye michuano mikubwa ya Klabu Bingwa Dunia, ambayo walimaliza katika nafasi ya tatu huku Bayern Munich ya Ujerumani ambayo iliwafunga mabao 2-0 katika mechi ya nusu fainali wakiibuka mabingwa.

Lakini pia Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa na kumbukumbu nzuri ya kuwachapa mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika kwa bao 1-0 kwenye mechi ya hatua kama hiyo msimu wa 2018/19 baada ya mchezo wa awali nchini Misri 'Wekundu wa Msimbazi' hao kuangukia kipigo cha mabao 5-0.

Tayari mashabiki wa Simba wamekuwa wakieleza matumaini yao makubwa kwa timu hiyo kuibuka na ushindi katika mechi zake za nyumbani ikiwa ni pamoja na ijayo dhidi ya Al Ahly, kutokana tu na rekodi nzuri ya kushinda ikiwa nyumbani kwenye mechi za kimataifa kwa miaka ya hivi karibuni.

Hata hivyo, pamoja na Simba kuwa na rekodi nzuri ya kutopoteza mechi za kimataifa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa miaka ya hivi karibuni, bado hiyo haiwezi kuwa sababu kwa wawakilishi hao wa Tanzania kubweteka kwa kutofanya maandalizi ya kina kuelekea mchezo huo ambao kwetu sisi tunauona ndio mgumu zaidi katika kundi lao.

Tumelazimika kutoa tahadhari hiyo mapema kwa wachezaji wa Simba, viongozi na hata mashabiki kwa kuwa sisi tunaamini rekodi katika soka zipo kwa ajili ya kuvunjwa, ndiyo maana Wekundu wa Msimbazi hao kwa mara ya kwanza katika hatua ya makundi ya michuano hiyo wameweza kuibuka na ushindi tena kwa kuifunga AS Vita ambayo nayo ilikuwa na rekodi nzuri zaidi ya kutopoteza ikiwa nyumbani tena dhidi ya timu kutoka Tanzania.

Nipashe hatuna shaka dhidi ya Simba pindi linapokuja suala la kujipanga ndani na nje ya uwanja katika mechi za kimataifa, lakini tunataka kuona ikifanya maandalizi makubwa zaidi na ya kina yatakayowapa matokeo chanya dhidi ya Al Ahly ili kujiweka mapema katika nafasi nzuri zaidi ya kufuzu hatua ya robo fainali.

Tunatambua kama Simba ikishinda mechi hiyo ya pili, tayari itakuwa na pointi sita hivyo itakuwa ikihitaji takriban pointi nne tu katika mechi zake nne zilizobaki mbili zikiwa za nyumbani na mbili za ugenini, jambo ambalo linawezekana.

Kubwa zaidi tunalotamani kuona likitokea ni Simba kutinga robo fainali ili kuiongezea Tanzania pointi na kuiwezesha msimu ujao wa kuingiza timu nne mbili Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho, kwenye michuano hiyo ambayo yote huandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

# Muungwana Lazima Nilonge

## Tatizo Yanga, Mbeya City si mwamuzi, zijimulike

**MARA** baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Yanga dhidi ya Mbeya City kumalizika, zilizuka vurugu kubwa zilizosababishwa na mashabiki wa timu hizo.

Ni vurugu zilizotulizwa na askari polisi kwa kutumia gari la maji ya kuwasha kutawanya mashabiki.

Mashabiki wa Yanga na Mbeya City wote walikuwa wakimlaumu mwamuzi Ludovic Charles kuwa hakuwatendea haki huku wale wa Mbeya City wakimlaumu mwamuzi huyo kwa madai kuwa aliwapa Yanga bao ambalo kwao waliamini mpira haukuvuka mstari.

Hilo lilikuwa ni bao la Deus Maseke kwenye dakika ya 85 ambalo pamoja na kuokolewa na Babilas Chitembe, lakini mpira tayari ulikuwa umevuka mstari wa goli.

Nao mashabiki wa Yanga walikuwa wakiilalamikia penalti walioipata Mbeya City kuwa haikuwa halali. Lakini ukiangalia marudio ya picha za video inaonekana bao la Yanga lilikuwa ni sahihi. Mpira ulikuwa umevuka mstari. Na hata penalti iliyopatikana kwa Mbeya City ilikuwa ni halali kwa sababu inaonekana kabisa mpira umemgonga mkononi beki, Yassin Mustapha.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze na Kocha Mkuu wa Mbeya City, nao pia wakaingia kwenye mtego wa mashabiki wao. Nao, pamoja na mambo mengine, wakamlaumu mwamuzi huyo kwa kila mmoja kudai kuwa timu yake haikutendewa haki.

Hata hivyo, ukiangalia uchezeshaji mzima wa mwamuzi huyo huoni kosa lake. Kila kitu kilicholalamikiwa hakikuwa sahihi. Labda ni makosa machache tu ya kawaida ambayo yapo kwa kila mwamuzi. Lakini goli la Yanga na penalti ya Mbeya City, vyote vilistahili. Tatizo ni kwamba makocha na mashabiki wao walitaka moja wapo kati ya hilo lisiwapo kwa wapinzani wao. Yanga walitaka bao lao liwe sahihi, lakini penalti isiwe sahihi. Mbeya City nao walitaka penalti yao ikubaliwe, lakini si bao la Yanga.

Ukichanganya na kuwa mabao hayo yalifungwa dakika za mwisho ndiyo kabisa yalizidi kuwachanganya mashabiki hao. Bao la dakika tano kabla mechi kumalizika, na la dakika tatu za nyongeza lililofungwa kwa penalti na Pastory Athanas, liliwafanya mashabiki kupagawa na kushindwa kuamini kinachotokea uwanjani.

Nadhani mashabiki wa Yanga baada ya bao lile, walidhani kazi imekwisha, bila kujua kuwa mpira wa miguu hauishi mpaka filimbi inapopulizwa.

Nafasi ambayo Yanga ipo, na ile ambayo Mbeya City ipo, ndiyo ilisababisha jazba kwa mashabiki wa timu zote mbili.

Yanga ipo kileleni ikiwa na pointi 45. Kabla ya mechi hiyo ilikuwa na alama 44 na ilizihitaji pointi tatu kwa udi na uvumba ili izidi kuikimbia Simba yenye pointi 38, hasa baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 hivi karibuni dhidi ya Azam FC.

Mbeya City iko kwenye hatari ya kushuka daraja ikiwa na pointi 15, nafasi ya 17. Na kabla ya mechi hiyo ilikuwa na pointi 14, hivyo ilihitaji pointi tatu ili kujivuta juu kidogo ya msimamo. Ndiyo maana utaona kila timu ilikamia na kuzitaka pointi tatu kwa udi na uvumba.

Ninachokiona hapa ni kwamba timu zote hizi zina upungufu makubwa ambayo wanayaficha kwa kivuli cha mwamuzi.

Mbeya City iko nafasi moja tu kutoka mkiani. Inashangaza kwani kwa mpira iliyocheza jana, ni ajabu kuona inadondosha pointi nyingi ikicheza na timu nyingine.

Kwenye mechi 19, Mbeya City imeshinda mbili tu, sare tisa na kupoteza nane. Hapo ndipo viongozi, makocha, wachezaji na mashabiki wa Mbeya City ilibidi watatue tatizo na si kumlaumu mwamuzi ambaye alionekana kuumudu mchezo huo.

Kwa upande wa Yanga, kocha Kaze anatakiwa kuinoa safu yake ya ushambuliaji ambayo inaonekana ni butu na si kuanza kumlaumu mwamuzi.

Kama washambuliaji wa Yanga wangekuwa makini, wangefunga mabao zaidi ya matatu, na lile la Mbeya City ingekuwa tu la kufutia machozi, lakini inaonekana kuwa imekuwa sasa ni tabia ya Yanga kufunga bao moja kwenye mechi nyingi, ikidhani inatosha kumaliza mechi.

Mimi nadhani timu hizi na makocha wake, wanaficha upungufu yao kwa kumlaumu mwamuzi ambaye hakuwa na baya kwenye mechi hiyo na kama yapo basi ni madogo ya kibinadamu lakini si kwa mabao hayo ya pande zote mbili.

HABARI KITAIFA

# WCF yalipa fidia bil. 23/- waathirika 5,700 miaka 4

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umelipa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 23 kwa waathirika wapatao 5,700 kuanzia Julai mwaka 2016 hadi kufikia Desemba 2020.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Masha Mshomba, alisema hayo mjini Morogoro katika hotuba yake wakati akimkaribisha Naibu Waziri wa Nchi ,Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Patrobas Katambi.

Alisema moja ya mafanikio ya Mfuko huo tangu kuazishwa Julai Mosi, 2015 hadi sasa kwa kiwango kikubwa yamechangiwa na kuanzishwa kwa huduma za mtandao na kuongezeka kwa malipo ya fidia ambayo ndiyo lengo hasa la kuanzishwa kwa mfuko huo.

Mshomba alisema wastani wa malipo ya fidia kwa mwaka ni zaidi ya Sh. bilioni 4.55 ni kuanzia 2016/2017 hadi 2020 na kuna tathmini inaendelea kufanyika kuwa ongezeko la malipo ya fidia kwa waathirika kuongezeka yataongezeka zaidi katika miaka ijayo.

"Tulianza kulipa fidia 2016/2017 hadi Desemba 2020 zaidi ya Sh. bilioni 23 zimelipwa na ukichukulia ile miaka minne ya kwanza ni zaidi ya Sh. bilioni 18 na ndiyo maana ninasema wastani wa kulipa fidia imekuwa wastani wa zaidi ya Sh. bilioni 4.55 kwa mwaka, " alisema Mshomba.

Alisema kwa sasa moja ya vipaumbele vya usoni ni kujenga uwezo wa kifedha kwa Mfuko ili malipo ya fidia yaweze kulipwa bila kutengemea msaada wowote.

Alisema pamoja na kulipa fidia, Mfuko umeweka kipaumbele kuendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi na waajiri ili wahakikishe kuwa mazingira yao ya kazi yanakuwa salama . Alitaja maeneo ya kazi wenye mazingira hatarishi ni sehemu za migodini, Kilimo na usafirishaji ambayo ajali ni nyingi na hata kwenye takwimu za malipo ya fidia kwenye sekta hizo zimekuwa zikiongoza.

Alisema Mfuko umeboresha huduma za tathmini kwa kutoa mafunzo kwa madaktari wapatao 1,085 ambao ndio wanaofanya kazi ya kutathmini kabla ya uliopaji wa fidia na mafunzo hayo yatakuwa ni endelevu .

Katika hatua nyingine, alisema Mfuko huo umejenga uwezo wa kutosha kwa mujibu wa hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) kufikia Juni 30, 2020 ukiwa na ukubwa wa thamani (Assets) Sh. bilioni 333, lakini pia hesabu ambazo hazijakaguliwa na CAG hadi Desemba 2020 imefikia Sh. bilioni 389.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), Hery Mkunda, alisema Mafanikio yaliyopatikana WCF ni kutokana na wafanyakazi kufanya kazi kwa kujituma kushauri vizuri uongozi na kushirikishwa katika masuala mbalimbali yanayohusu taasisi.

Mkunda ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), alisema; "Niipongeze Menejimenti na kuwaomba waajiri wengine kujifunza kutoka WCF, hawa wafanyakazi ndio walio jikoni wanaweza kushauri vizuri kuhusu masuala mbalimbali inayohusu taasisi ili kufikia malengo."




Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo (katikati), akiwa pamoja na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Maiputa, Benson Ndosi (kulia) na Mkurugenzi wa Taasisi ya Voefowo, Asifiwe James, baada ya kuzindua mradi wa kupanda miti ujulikanao kama 'Tigo Green for Kili', wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro juzi, ambapo miti 10,000/- itapandwa ili kulinda hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## WLAC yawaeleza waajiri haki, maslahi wa wafanyakazi wao

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), kimewataka waajiri kuangalia maslahi na haki mbalimbali wanazostahili kutoka kwa wafanyakazi wao.

Mratibu wa mradi wa kuwawezesha wanawake na vijana kutoka WLAC, Consolata Chikoti, alisema pamoja na kuwapo kwa sheria zinazolinda haki za wafanyakazi, lakini kumekuwa na tabia kwa baadhi ya waajiri kuzikiuka ikiwa ni pamoja na kushindwa kutoa haki zinazostahiki kupewa wafanyakazi.

Alisema zipo haki mbalimbali ambazo waajiri wamekuwa wakizikiuka kwa wafanyakazi wao ikiwamo kuvunja mikataba yao kinyume cha taratibu na sheria za ajira.

Akizungumza katika semina iliyoandaliwa na Kituo hicho kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi, Chikoti alisema, bado pia kuna tatizo kwa wafanyakazi wengi kushindwa kutambua haki zao mbalimbali wanapokuwa kazini au mikataba yao ya ajira kukatishwa.

"Na ndio maana tunafanya semina kama hizi za kuwajengea uwezo wafanyakazi katika sekta mbalimbali namna ya kutambua haki zao na kuzisimamia zinapokiukwa,"alisema Chikoti.

"Lakini pia ni vema hata waajiri nao wakazingatia yale ambayo sheria inawataka kufanya kuhusu wafanyakazi wao, waache kuwakatishia mikataba kwa visingizio ambavyo vinakiuka haki za binadamu na ambavyo havina utu ndani yake."

Chikoti alisema tatizo la ukiukaji wa sheria na taratibu za ajira za wafanyakazi halipo tu katika sekta binafsi bali pia katika sekta ya umma.

Baadhi ya washiriki wa semina hiyo akiwamo Bundi Clement kutoka kiwanda cha kuzalisha vinywaji cha SBC, alisema wafanyakazi wengi wamekuwa wakishindwa kudai na kusimamia haki zao pale zinapokiukwa na waajiri wao kwa sababu ya kuogopa kufukuzwa kazi.

"Ukweli ni kwamba watu wengi huwa hawana ujasiri wa kuhoji pale haki zao zinapokiukwa, kwa mfano wanaofanya kazi viwandani, wengi wao mikataba wanapewa ya muda mfupi, kwa hiyo hata kama mwajiri wake anamuonea hawezi kuhoji kwa sababu anaogopa kwamba mkataba wake ukiisha hapewi tena, kwa hiyo wengi wanakuwa wanaumia lakini hawawezi kusema," alisema Clement.

## Kiwanda kipya kuwa fursa sekta ya ngozi

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANDA kipya cha ngozi ambacho uwekezaji wake umegharimu mabilioni ya fedha kilichozinduliwa na Rais John Magufuli mwishoni mwa wiki mkoani Morogoro, kitazalisha bidhaa za ngozi zenye viwango vya kimataifa.

Kadhalika, kinatajwa kusaidia kuongeza mnyororo wa thamani wa ngozi nchini kutoka kwenye machinjio hadi kwenye soko.

Kiwanda hicho ambacho awali kinajulikana kama ACE Leather Tanzania Limited, kinaendeshwa na Kampuni ya Taifa Leather Company Limited, kwa sasa ndicho kiwanda kikubwa zaidi cha kusindika ngozi barani Afrika na kinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100 ambao wamefanya uwekezaji mkubwa.

Akizungumza katika mahojiano maalum baada ya uzinduzi uliofanyika kiwandani hapo kilichopo maeneo ya Kihondo, Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Onorato Garavaglia, alisema Taifa Leather Company Limited imewekeza Sh. bilioni 50 za Kitanzania katika awamu ya kwanza na ya pili ya ukarabati wa kiwanda, na kwamba uwekezaji huu utawezesha bidhaa bora za kampuni kushindana kwenye ngazi ya kimataifa.

# Bashiru ataka sheria kali wanaodhalilisha wanawake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameonyeshwa kukerwa na tabia ya watu kuwatuhumu viongozi kuwa wamekuwa wakitoa nafasi za uongozi kwa wanawake kwa upendeleo kutokana na mahusiano waliyonayo.

Kutokana na hilo, ameshauri kutungwa kwa sheria kali dhidi ya udhalilishaji wa wanawake.

Dk. Bashiru alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumza katika semina ya wabunge wanawake wa CCM iliyofanyika Jijini hapa.

Alisema tabia hiyo haipaswi kufumbiwa macho kwa sababu kwenye jamii ya baadhi ya watu wapo wanaoamini kwamba mwanamke hawezi kupata nafasi kwa haki bila kupendelewa kwa sababu ya mahusiano ya mtu.

Katibu huyo alisema wanawake hawapaswi kuendelea kuvumilia kashfa hizo zenye kuwadhalilisha, hivyo wanapaswa kuwa na misimamo mikali dhidi ya vitendo hivyo.

"Lipo tatizo jingine kwenye jamii la baadhi ya watu kutoamini kwamba mwanamke anaweza kupata nafasi kwa haki bila kupendelewa, na wakati mwingine kukashfiwa kuwa amependelewa kwasababu ya mahusiano na mtu fulani mwanaume, mimi mmoja wapo muathirika wenu na ninasikitika kweli, hata Rais wetu ni muathirika pia,,"

"Nilipokuwa chuo kikuu nimekaa zaidi ya miaka 15 sikuwahi kuhisiwa kwamba nina upendeleo kwa wanafunzi wangu wa kike, lakini kwenye Chama hapa, ni kichefu chefu. Naelewa ni mazoea kwamba mwanamke akifanikiwa lazima atafutwe mtu aliyembeba na na huyo sio kumbeba kwa sifa yake ni kumbeba kwa kumpendelea,"alisema.

Alisema yamejengeka mazoea kuwa mwanamke akifanikiwa lazima atafutwe mtu aliyembeba na si kumbeba kwa sifa yake bali kumpendelea.

"Hili tatizo ambalo mkilivumilia linawadhalilisha, nadhani sheria zetu tuziangalie upya kama tumekuwa na sheria kali dhidi ya makosa ya ubakaji na jinai za ubakaji, lazima tuwe na sheria kali dhidi wanaokashifu wanawake ili watu waache kuropoka na kuzua mambo ambayo hayapo, hayana ushahidi lakini yanadhalilisha mwanamke ili aonekane hafai, aonekane akipata nafasi kabebwa na kabebwa kwa kukashifiwa,"alisema.

Aidha, alisema baadhi ya wanawake pia wamekuwa sehemu ya kueneza maneno ya kuwadhalilisha wanawake wenzao kwenye jamii.

"Mwenyezi Mungu amenijaalia watoto wa kike pekee, kwa hiyo nikiwaangalia wanangu wanavyohangaika, tunavyohangaika pamoja, ninavyowahimiza, walivyo na tamaa ya kufanya vizuri, halafu waje wadhalilishwe na kukashfiwa kwamba mafanikio yao ni yakubebwa," alisema.

Pamoja na hayo, alisema wanawake wamepewa mzigo mzito ambao ni lazima wathibitishe kwamba uwezo wao ni sawa na wanaume na wakati mwingine ni zaidi ya wanaume ili kusaidia kujenga hoja kwa watu ambao imani yao ni ndogo kwa wanawake.

Alisema taifa bado linategemea mchango wa wanawake, hata hivyo mchango wao bado haujionyeshi katika kiwango cha maendeleo yao.



Meneja wa maduka ya Total, Jane Mwita, akizungumza wakati wa kuadhimisha Siku ya Wapendanao iliyofanyika jana ambapo kila aliyejaza mafuta kituo cha Total alipatiwa zawadi ya Ua la Upendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Total yatoa zawadi kwa wateja wake

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya mafuta ya Total imepunguza bei kwa baadhi ya bidhaa zinazouzwa katika maduka yake (Super market) ikiwamo ya 'Chocolate' kwa kuiuza Sh.2800 mbili, kutoka Sh.4000 iliyokuwa ikiuzwa awali.

Pia, wanatoa huduma bure kwa wateja wanaojaza mafuta katika vituo vyao kwa kuwaoshea gari bure pamoja na kuwapatia zawadi mbalimbali ikiwamo za maua.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa bidhaa katika maduka ya kampuni hiyo, Jane Mwita, alisema punguzo la bidhaa na utoaji wa huduma hizo ni mpaka Februari 28, mwaka huu.

Alisema lengo ni kutaka wateja wao wafurahie msimu wa wapendanao kwa kuwanunulia zawadi kwa kutumia fursa ya punguzo katika bidhaa hizo ambazo zinapendwa na wengi.

"Tumepunguza bidhaa zetu katika msimu huu wa wapendanao mpaka Februari 28, mwaka huu, tunataka wateja wetu wafurahie kwa kadri watakavyo, wanunue za kutosha kwa ajili ya watu wanaowapenda na kusiwe na kikwazo cha fedha,"alisema Mwita.

"Na tunaamini kwamba punguzo hili litawafaa watu wa makundi yote, vijana, rika la watu wa kati na hata wazee, kwa sababu tumaanimi vitu kama hivi hufanywa kwa upendo na kwa kuonyesha moyo wa kuthamini."

Alisema kampuni hiyo ya Total, itahakikisha inaendelea kujipanga katika matukio tofauti yanayojitokeza katika jamii na kushiriki ili kurudisha shukurani kwao.

"Sisi ni miongoni mwa kampuni ambayo tumekuwa kukithaminiwa sana na Watanzania, kwa hiyo ili kurudisha shukrani yetu kwao, tutahakikisha tunashiriki kikamilifu katika matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii na hiyo ndio itakuwa fadhila yetu kwao,"alisema Mwita.

Baadhi ya wateja waliofika kupatiwa huduma na kununua bidhaa hizo za punguzo, waliipongeza kampuni hiyo kwa kushusha bei kwa baadhi ya bidhaa zilizo katika maduka yao.

"Utaratibu huu ambao wameanzisha Total ni mzuri, wameona angalau mara moja moja na wao wawafurahishe wateja wao kwa kutoa ofa kwenye bidhaa, mimi sikujua kama nitakutana na kitu kama hiki na nashukuru imekua kama suprise na nimefurahia, nimenunua Chocolate za kutosha kwa ajili ya wapendwa wangu na naamini watafurahia sana kwa sababu wanazipenda,"alisema Elizabeth Amuli.

Benjamin Saimon, alisema utaratibu huo ni mzuri na ni vema kampuni nyingine zikaiga hususani kutoa baadhi ya huduma kwa jamii.

# AMCOS 85 zafutiwa usajili ununuzi mazao

**Na Said Hamdani,** LINDI

VYAMA vya Msingi na Ushirika (AMCOS), 85 vilivyosajiliwa kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima, mkoani Lindi, vimefutwa.

Vyama hivyo ni kati ya 115 ambavyo vilisajiliwa kufanya shughuli hiyo. Ofisa Ushirika Mkoa wa Lindi, Projestus Thomas, aliyasema hayo katika mahojiano maalum na NIPASHE, ofisini kwake mjini hapa.

Thomas alisema sababu mojawapo ya vyama hivyo kufutwa ni kukiuka taratibu, kushindwa kufanya kazi ikiwamo Sheria ya Ushirika.

Alisema vyama hivyo vimefutwa tangu Aprili, mwaka 2019 baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Januari 2019, kwa madai ya kushindwa kutekeleza matakwa ya kisheria ya ushirika, kutofanya kazi tangu kusajiliwa, kutokuwa na ofisi wakiwemo na wanachama.

"Baada ya mamlaka kuvifuta vyama 85, Mkoa tumebakiwa na vyama 30 vinavyoendelea na kazi za kuhudumia wakulima," alisema Thomas.

Alifafanua kwa kutaja idadi ya vyama vilivyofutwa kwa kila Halmashauri ikiwamo, Kilwa 24 kati ya vilivyokuwapo 28, Nachingwea 23, Mtama 19, Liwale 10 na Lindi Manispaa saba.

Aliongeza kuwa vyama hivyo vimefutwa chini ya Sheria namba 6/2013 kifungu cha 100 kifungu kidogo cha pili, baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali mwezi Januari, 2019.

Ofisa Ushirika huyo Mkoa, alisema Ofisi yake imepokea maombi matano mapya, kutoka halmashauri ambazo ni Ruangwa, Mtama kila moja ikiwasilisha maombi mawili, wakati Lindi Manispaa ikiwasilishwa ombi moja na kwamba mchakato umeanza wa kupata leseni kwa njia ya mtandao.

HABARI KITAIFA

## Tigo, Samsung sasa zazindua simu mpya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tigo Tanzania imeungana na Kampuni ya simu ya Samsung kuzindua simu mpya aina ya Samsung Galaxy S21+ na Samsung Galaxy S21 Ultra katika soko la Tanzania.

Hatua hiyo imeelezwa ni sehemu ya mkakati wa kampuni kuongeza kasi ya matumizi ya mtandao wa 4G nchini.

Meneja wa bidhaa za intaneti wa Tigo, Mkumbo Muyonga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa simu hizo mwishoni mwa wiki, alisema: "Tunafuraha kuwa kampuni ya kwanza ya mawasiliano kupokea na kuuza Samsung Galaxy S21, Samsung Galaxy S21+ na Samsung Galaxy S21 Ultra katika soko la Tanzania.

Huu ni uthibitisho wa imani kubwa ambayo wadau wetu wanayo juu yetu kama msambazaji mkubwa, mtandao mkubwa wa 4G, ofa mbalimbali pamoja na timu ya huduma kwa wateja amnbayo inahakikisha wateja wetu wanapata huduma za hali ya juu kila wakati."

Aliongeza kuwa lengo lao ni kuchochea maisha ya kidigitali Tanzania na ndio maana wameungana na Samsung kuongeza idadi ya watumiaji wa simu janja na mtandao nchini.

Alisema wamezizatiti katika kuwawezesha Watanzania kupata teknolojia za kisasa zaidi na ndiyo maana wanatoa zaidi ya GB 78 za intaneti kwa mwaka mzima kwa wateja wanaonunua simu za Samsung Galaxy S21+ na Samsung Galaxy S21 Ultra.

Muyonga alisema Tigo inaendelea kuchochea ueneaji na utumiaji wa simu janja nchini kwa kuhakikisha wateja wake wanafurahia ulimwengu wa kidigitali kupitia mtandao wenye kasi zaidi wa 4G kutoka Tigo ambao ni mkubwa zaidi nchini.

Akizungumzia muungano huo, Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed, alisema: "Simu hii mpya ya Galaxy S21 5G series imetengenezwa mahususi kwa ajili ya kumpa mtumiaji uzoefu wa kipekee zaidi ambao utafanya kila siku kuwa nzuri zaidi. Galaxy S21 series imeundwa kwa teknolojia za kisasa zaidi zinayoipa uwezo wa kuwa na spidi zaidi pamoja na muonekano wa kipekee."

**Lengo lao ni kuchochea maisha ya kidigitali Tanzania na ndio maana wameungana na Samsung kuongeza idadi ya watumiaji wa simu janja na mtandao nchini.**

# Vijiji vyanufaika na bilioni 2/- za mgodi

**Na Samson Chacha,** TARIME

KAMPUNI ya Twiga kupitia mgodi wa dhahabu ya Barrick North Mara uliopo Nyamongo wilayani Tarime mkoani Mara, umetoa Sh. bilioni 2 kwa ajili ya malipo ya ushuru wa huduma kwa Halmashauri ya Tarime Vijijini.

Aidha, mgodi huo huo umechangia katika shughuli za miradi ya maendeleo katika vijiji 11 vinavyouzunguka.

Hundi ya fedha hizo ilipokelewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo ya Tarime Vijijini, Saimon Kres na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Apoo Tindwa, kamati ya Ulinzi na usalama ya wilaya hiyo pamoja na madiwani wa Halmashauri hiyo katika Ofisi za Halmashauri hiyo Kijiji cha Nyamwaga Tindwa alisema aliipongeza

Kampuni ya Twiga kupitia mgodi huu wa Barrik North Mara kwa kutimiza ahadi zake za kulipa ushuru na kodi mbalimbali kwa Halmashauri na kuchangia katika miradi ya maendeleo katika vijiji 11 vinavyozunguka mgodi huo.

**Fedha hizi walizotoa kwetu Sh. bilioni 2 ni malipo ya kuanzia Julai 2020 hadi Desemba 2020, na ni malipo endelevu kwa Halmashauri yetu kutoka katika mgodi huo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.**

"Fedha hizi walizotoa kwetu Sh. bilioni 2 ni malipo ya kuanzia Julai 2020 hadi Desemba 2020, na ni malipo endelevu kwa Halmashauri yetu kutoka katika mgodi huo kwa ajili ya miradi ya maendeleo," alisema Tindwa.

Akikabidhi hundi hiyo, Meneja Mkuu wa Mgodi Barrick North Mara, Luiz Correin, alisema mgodi unaona fahari kutekeleza makubaliano na Halmashauri ya Tarime Vijijini kwani fedha hizo zinatumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa madarasa , zahanati , nyumba za walimu, maji na miundombinu ya barabara.

"Malipo ya fedha hizo ni endelevu kwa ajili ya kuimarisha huduma za kijamii katika Halmashauri, tunaomba ushirikiano huo uendelee kuwapo kwa pande zote mbili kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi," alisema Correin.

Naye Mwenyekiti Kres alisema Halmashauri imepitisha rasmu ya bajeti ya shilingi 38,273,963,588.36 kwa kipindi cha 2021 /2022 ukilinganisha na ya mwaka 2020/2021 ya shilingi 34, 825,488,137.00, ambapo baraza la madiwani liliazimia kila kata kupata mgawo wa Sh. 60,000,000 kwa ajili ya kuendeleza miradi katika kila kata ikiwamo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, zahanati , maji na barabara.

" Tunatarajia kununua greda kwa ajili ya barabara na kulipa deni la Sh. 185 ,000,000 kwa Bohari Kuu ya Dawa tulizokuwa tunadaiwa ili kupata dawa ya kusambaza katika vituo vyetu vya afya na zahanati," alisema Kres.



Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) kinachomilikiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Aristid Kanje (Kushoto), akionyeshwa namna ya kuendesha ndege isiyo na rubani na wahitimu wa Mafunzo ya Ndege nyuki 'Drone' wakati wa kuwatunuku vyeti jijini Dar es Salaam. Wahitimu 15 walihitimu mafunzo hayo kwa awamu ya pili ya wiki nne. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sababu ajali kupungua Kaskazini Pemba

**Nas Mwandishi Wetu,** PEMBA

WATU 27 wamefariki dunia na wengine 38 kujeruhiwa kufuatia ajali 63 zilizotokea katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kuanzia Januari mwaka 2019 hadi Disemba 2020.

Mwaka 2020 zilitokea ajali 30 zilizosababisha vifo 13 na kujeruhi 18 ambapo mwaka 2019 zilitokea ajali 33 zilizosababisha majeruhi 20 na vifo 14.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alieleza kuwa mwaka 2020 ajali zilipungua ukilinganisha na mwaka 2019.

"Katika mwaka 2020 ajali zilipungua kidogo kutokana na kuendelea kutoa elimu kwa madereva na wananchi katika wilaya zote mbili ili kudhibiti wimbi la ajali na vifo vitokanavyo na ajali," alisema Kamanda huyo.

Kamanda Sadi alifahamisha kwa mwaka 2021 Jeshi la Polisi limejipanga vizuri kuhakikisha ajali za barabarani zinaoungua.

Alieleza kuwa kitengo cha Usalama Barabarani Mkoa kimekuwa kikifanya zoezi maalumu la kuwapina madereva kwa kutumia chombo maalumu cha kupimia mwendo pamoja na madereva wote ambao wanalewa, huku wakiwa wanaendesha gari.

"Juhudi kubwa zinazofanywa na Jeshi la Polisi, ili kuhakikisha ajali zinapungua ni kufanya zoezi mara kwa mara barabarani la kuwakamata madereva wote wazembe, ambao wanaendesha vyombo kwa kasi au wengine wanalewa, huku wanaendesha magari," alifafanua Kamanda Sadi.

"Lakini pia katika matukio hayo ajali nyingi huwa zinasababishwa na waendesha boda boda licha ya kuwa bado hakujawa na sheria rasmi ya bodaboda, lakini inavyoonekana wamepewa ruhusa ya kufanya shughuli hiyo ya kuchukua abiria," alieleza Kamanda Sadi.

# Mradi wa maji wanufaisha 70,000

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI 70,000 kutoka vijiji 20 katika Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga na Ushetu mkoani hapa, wanatarajiwa kuondokana na shida ya kutumia maji machafu.

Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Julitey Payovela, alibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Bodi ya Zabuni ilipokagua utekelezaji wa miradi ya maji.

Alisema katika miradi 12 ya majisafi na salama, ambayo wanaitekeleza hivi sasa katika vijiji 20 vya Wilaya ya Shinyanga na Ushetu yenye thamani ya Sh. bilioni 5.2 itatoa huduma ya maji kwa zaidi ya wananchi 70,000 na kuwaondolea shida ya kutumia maji machafu ambayo ni hatari kiafya.

**Miradi hii 12 ya maji safi na salama kwenye vijiji vyote hivi Ishirini ambayo tunaitekeleza hivi sana.**

"Miradi hii 12 ya maji safi na salama kwenye vijiji vyote hivi Ishirini ambayo tunaitekeleza hivi sana, ipo katika hatua ya ukamilishaji na mingine imeshaanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi, ambapo tunatarajia ifikapo mwezi March yote itakuwa imekamilika kwa asilimia 100," alisema Payovela.

"Ombi langu kwa wananchi waitunze miundombinu ya miradi hii ya maji ili idumu kwa muda mrefu na kutoa huduma ya maji safi na salama, sababu Serikali inatumia fedha nyingi kuwatekelezea miradi ili kuwafanya wawe na maisha bora na kufanya shughuli zao za kiuchumi bila ya kuugua ovyo sababu ya kunywa maji machafu," aliongeza.

Alisema katika mwaka wa fedha 2020/2021 walitenga kiasi cha fedha Sh. Bilioni 12, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, ambapo lengo la Serikali hadi ifikapo mwaka 2025 wananchi wa vijijini wawe wameshapata majisafi na salama kwa asilimia 85.

Naye Mwenyekiti wa bodi hiyo ya Zabuni Rubeni, Mwandubya, alisema wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maji safi na salama kwa wananchi ambayo inatekelezwa na RUWASA, baada ya kujionea miradi mingi ipo katika hatua ya ukamilishwaji na mingine imeanza kutoa maji.

Baadhi ya wananchi ambao ni wanufaika wa miradi hiyo ya maji, akiwamo Aziza Joseph kutoka kijiji cha Masengwa wilayani Shinyanga, waliishukuru kutekelezewa miradi ya maji safi na salama, ambayo itawasaidia kuondokana na kupoteza muda wa kufanya shughuli za kiuchumi sababu ya kufuata maji umbari mrefu.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti (kushoto), akipokea msaada wa mabati kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (wa pili kulia) katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika mwishoni mwa juma katika shule ya sekondari Galapo wilayani Babati mkoani Manyara.Wengine ni Meneja Mahusiano ya Serikali wa NMB Kanda ya Kati, Peter Masawe (wa pili kulia) na Meneja wa NMB Tawi la Babati, Antiphas Nnko (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yagawa mabati 950 shule 6 Babati

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

Benki ya NMB imetoa msaada wa mabati 950 kwa ajili ya shule sita za sekondari zilizopo Wilayani Babati ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Serikali katika ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Makabidhiano hayo yalifanyika mwishoni mwa juma katika Shule ya Seondari Galapo wilayani Babati na mgeni rasmi katika makabidhinao hayo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema msaada huo ni kuunga mkono juhudi za Serikali kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Msaada huu tuliokabidhi leo ni kuunga mkono juhudi za serikali yetu katika kuhakikisha kuwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wanaingia madarasani bila kukosa," alisema .

Mlozi alitaja thamani ya mabati hayo yaliyotolewa kuwa ni zaidi ya Sh. milioni 28.1 kwa jili ya shule sita za sekondari zilizopo wilayani hapa.

Shule zilizofaidika na msaada huo ni Magugu, Galapo, Madunga, Nar, Qash na Aytesea.

Aidha, alisema Nmb imekuwa ikitoa misaada kwenye jamii huku lengo kuu ni kurudisha fadhila kwa jamii kutokana na faida inayoipata kila mwaka kwasababu ya wananchi kuunga mkono benki katika kutumia huduma za kifedha wanazotoa.

Kadhalika, alisema misada hiyo imekuwa ikielekezwa kwenye maeneo muhimu ya kutolea huduma za kijamii hasa sekta ya afya,elimu na wakati wa majanga .

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa Halmshauri ya Babati Vijijini, John Nchimbi, aliwashukuru NMB kwa msaada waliotoa, huku akisisitiza kuwa benki hiyo imekuwa ni mkombozi kwa wananchi wanyonge kutokana na kutoa misaada hiyo

Nchimbi alisema msaada uliotolewa umewapunguzia mzigo wazazi kwani wagetakiwa kuchangia ujenzi huo wa madarasa ambao unagharimu fedha nyingi.

Alisema baada ya msaada huo wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 503 ambao walioshindwa kujiunga na masomo atakuwa na uhakika wa kuingia darasani wiki ijayo na walikuwa na upungufu wa vyumba 13 katika Halamshauri hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Joseph Mkirikiti alizitaka kamati za shule kuhakikisha wanatafuta mafundi bora wa kupaua mapaa ya mabati ili kuepuka kuharibu mabati wakati wa ujenzi.

Mkirikiti alisema NMB wameipunguzia serikali mzigo kwa kusaidia mabati kwaajili ya kupaua na hivyo kusaidia wanafunzi wengi watakaosoka katika shule hizo kwa vizazi vijavyo kwani shule zinakaa na kuhudumia watu wengi zaidi.

# Wazalishaji waliopata vyeti ubora wafundwa

**Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wazalishaji waliopata vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora kuwa mabalozi kwa kuendelea kuzalisha bidhaa zenye viwango ili wawe chachu kwa wengine kufika katika shirika hilo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, wakati wa kukabidhi vyeti na leseni kwa wazalishaji ambao bidhaa zao zimethibitishwa kukidhi matakwa ya viwango.

Miongoni mwa waliopata vyeti na leseni hizo ni wazalishaji wa bidhaa za chakula, vipodozi, vilainishi, vitakasa mikono, vifaa vya umeme, vibebo, vifungashio na vinginevyo.

Alisema vyeti na leseni walizopata zinafanya bidhaa zao kukubalika sokoni, hivyo ni fursa nzuri ya wao kuhimili soko la ushindani popote pale.


"Vyeti na leseni hizi ni kibali cha kuingiza na kuuza bidhaa zenu katika soko la Afrika mashariki na nje ya hapo na kuweza kushindana," alisema.

Aidha, alisema leseni na vyeti hivyo vinasaidia bidhaa zilizothibitishwa kuongeza imani kwa walaji, hivyo wataweza kuuza kwa wingi. Aliwataka wajasiriamali nchini kujitokeza kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha bure TBS kwa sababu gharama hizo zinalipwa na Serikali.

Alitoa mfano akisema kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita Shirika hilo limetumia Sh. milioni 550 kuthibitisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali bure.

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya baada ya miaka mitatu wajasiriamali wanatakiwa kulipa robo ya gharama, lakini ikibainika hawajawa na uwezo, TBS inaendelea kuwalea hivyo aliwataka kutunza kumbukumbu za mali wanazonunua na kuuza vizuri.

Nipashe
Spotika



WAFUNGAJI 10 BORA LIGI TANO ULAYA MSIMU HUU UK. 12 &13



Ilkay-gundogan

# VIUNGO WA5 EPL WALIOPIKU MATARAJIO YAO MSIMU HUU

**LONDON, England**

HUKU tukiwa nusu ya msimu wa Ligi Kuu England, tayari kuna wachezaji wameonyesha kwamba wanaweza kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka.

Bruno Fernandes ameendelea kuonyesha kiwango chake pale Manchester United na ameanza kuwa mchezaji muhimu dimbani, huku Harry Kane na Heung-min Son wameendelea kufunga kila wakiingia uwanjani.

Hata hivyo, makala haya yanawaangalia viungo kwenye Ligi Kuu England ambao wamewashangaza wengi kwa sababu tofauti kinyume na walivyotarajiwa, hawa hapa...

**#5. Wilfried Ndidi - Leicester City**

Manchester United ilionyesha nia ya kweli kabisa ya kutaka kumsajili Wilfried Ndidi, lakini abakia kuwa nguzo ya kocha Brendan Rodgers pale Leicester City.

Ndidi si jina geni kwenye Ligi Kuu England akiwa amecheza kwa miaka mitatu iliyopita, lakini kiwango cha Ndidi kimezidi kuimarika.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Nigeria amekuwa mchezaji muhimu mno kwa kikosi cha Leicester.

Katika umri wa miaka 24, bila shaka yoyote Ndidi ataendelea kuwa mmoja wa wachezaji bora kwenye nafasi yake duniani kama ambavyo anatamba kwa sasa.

**#4. Tomas Soucek - West Ham**

Ni mwaka sasa tangu Tomas Soucek aliposajiliwa kutoka Slavia Prague, na amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia mno, mchezaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Czech.

Akiwa anatajwa na David Moyes kama 'Marouane Fellaini mpya', Soucek amekuwa katika kiwango bora kabisa.

Tayari na mabao saba kwa jina lake katika mechi 20 za Ligi Kuu msimu huu, Soucek amekuwa nguzo kubwa sana kwa West Ham ambao wanapigania kufuzu kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Si wengi walitarajia Soucek angeweza kuwa na maisha mazuri nchini England, lakini amethibitisha tofauti kabisa, kwani kila nafasi anayoipata anaitumia vizuri sana.

Soucek anaweza kuwa mgeni kwenye Ligi Kuu England, lakini anacheza kama amekuwa kwenye EPL kwa muongo mmoja.

**#3. Tanguy Ndombele - Tottenham**

Mwanzo wake haukuwa mzuri sana kwa miamba hao wa London Kaskazini, lakini Tanguy Ndombele sasa amekuwa kwenye mipango ya Jose Mourinho.

Kwa sasa Ndombele anaonekana kuziteka vizuri akili za Mourinho na kuonekana kuwa ndio nguzo muhimu kwa kikosi hicho.

Mfaransa huyo alitua hapo Spurs kwa kiasi cha pauni milioni 50 na sasa ameonyesha ubora wake halisi.

Mashabiki sasa wamerudisha imani yao kwa Ndombele na sasa wanamtarajia kubakia kwenye klabu hiyo kwa miaka mingi inayokuja.

**#2. Pierre-Emile Hojbjerg - Tottenham**

Amekuwa kwenye EPL kwa miaka minne akiwa kule Southampton, wengi waliona ubora wake usioshuka wa Pierre-Emile Hojbjerg.

Lakini baada ya uhamisho wa pauni milioni 15 - ambao kwa sasa unaonekana kama usajili bora zaidi wa kipindi cha majira ya joto - raia huyo wa Denmark ameibuka na kuonyesha kiwango chake na kuwa sehemu ya mipango ya Mourinho.

Aina yake ya uchezaji wa kutumia akili zaidi umemfanya kutengeneza makosa machache sana na amekuwa akifanya kazi kubwa msimu huu.

Anaweza asiwe mchezaji anayevutia ikilinganishwa na mchezaji anayefunga mara kwa mara, winga au mshambuliaji, lakini jukumu la Hojbjerg namna gani anaisaidia Tottenham uwanjani ni kubwa mno.

Katika umri wake wa miaka 25, ndio kwanza anaingia kwenye muda wake bora zaidi na anaweza kuwa bora zaidi kwa miaka mingi inayokuja.

**#1. Ilkay Gundogan - Manchester City**

Wengi wamemuangalia Ilkay Gundogan kwa zaidi ya miaka wakati akiwa kule Borussia Dortmund na sasa akiwa Manchester City na wametambua ubora wake, lakini ni hivi karibuni tu ndio mashabiki wameelewa kwamba anaweza kucheza nafasi nyingi zaidi dimbani.

Anajulikana anacheza nafasi ya kiungo mkabaji, lakini Gundogan ameonyesha katika miezi miwili iliyopita kwamba ana uwezo wa kufunga na kuifanya Manchester City kuwa imara zaidi na zaidi.

Huku Kevin De Bruyne akiwa majeruhi, raia huyo wa Ujerumani amechukua nafasi yake na ameitendea haki bila kuonyesha pengo lolote, wakati pia akiendelea kuwa msaada kwenye ukabaji na ulinzi.

## ISIKUPITE

KATIKA mechi zote sita za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika zilizopigwa Ijumaa na Jumamosi, timu pekee iliyoibuka na ushindi ugenini ni Simba baada ya kushinda 1-0 dhidi ya AS Vita ya DR Congo, zingine zote ziliambulia kichapo isipokuwa CR Belouizdad na MC Alger ambazo zililazimisha sare tasa ugenini dhidi ya TP Mazembe na Zamalek. Matokeo mengine ES Tunis 2-1 Teungueth, Horoya 2-0 Petro de Luanda na Mamelodi Sundowns 2-0 TBD.



# SIMBA ILIVYOTETEMESHA AFRIKA




Straika wa Simba, Mkongomani Chris Mugalu, akipiga penalti iliyokwenda moja kwa moja wavuni na kuipatia timu hiyo bao pekee ugenini dhidi ya AS Vita kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi Ijumaa iliyopita. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

"HII ni Simba, ushindi wa kwanza ugenini kwenye historia ya Ligi ya Mabingwa Afrika ngazi ya makundi." Limeandika Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwenye mtandao wake wa kijamii kwa lugha ya Kiingereza, likiielezea timu ya Simba na ushindi wake wa bao 1-0 ilioupata dhidi ya AS Vita.

Usiku wa Ijumaa, Simba iliichapa AS Vita bao 1-0 kwenye Uwanja wa Martyrs mjini Kinshasa, likifungwa na straika mzaliwa wa nchi hiyo ya DR Congo, Chris Mugalu kwa mkwaju wa penalti dakika ya 61 BAADA YA shuti la Luis Miquissone kumgonga mkononi Qusmane Quttara kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mchezo wa Kundi A.

Ni ushindi ambao umeonekana pamoja na kuwafurahisha Watanzania wengi, lakini pia umewashangaza baadhi ya mashabiki wa soka Afrika, kwani ni nadra kwa AS Vita kufungwa kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Kwa ushindi huo, Simba imeweka rekodi ya kufunga mabao sita na kufungwa bao moja, huku ikicheza bila kuruhusu bao lolote kwenye mechi nne ilizocheza tangu kuanza kwa Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Ilianza safari yake kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Plateau United ya Nigeria kwa kuichaa bao 1-0 ugeini na mechi ya marudiano nchini ilimalizika bila kufungana.

Kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilichapwa bao 1-0 ugeini dhidi ya FC Platinum, lakini ikashinda mabao 4-0 mechi ya marudiano, kabla ya kuanza kwa kushinda bao 1-0 dhidi ya AS Vita hatua ya makundi.

Kwenye makala haya tunaziangalia rekodi kadhaa ambazo Simba imeweka kwenye michuano hii mpaka sasa kiasi cha wachambuzi wa soka barani Afrika kuanza kuiangalia kwa jicho la kipekee...

**#1. Ya kwanza kushinda makundi msimu huu**

Simba ndiyo timu ya kwanza kupata ushindi msimu huu kwenye hatua hiyo, kwani siku ya Ijumaa zilichezwa mechi mbili tu, nyingine ikiwa ni Zamalek ya Misri ikiwa nyumbani dhidi ya MC Alger ya Algeria na timu hizo kutoka suluhu bila kufungana.

**#2. Timu pekee iliyoshinda ugenini**

Mpaka sasa Simba ndiyo timu pekee iliyoshinda ugenini kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye ngazi ya makundi.

MC Alger ya Algeria ilishindwa kuifunga Zamalek ya Misri kwao na kwenda suluhu, Teungueth ya Senegal, ikaambulia kichapo ugenini cha mabao 2-1 kutoka kwa Esparence ya Tunisia, CR Belouidad ya Algeria ikashindwa kuifunga TP Mazembe kwao na kutoka suluhu, Petro de Luanda ikaambulia kipigo cha mabao 2-0 ugenini kutoka kwa Horoya ya Guinea na Al Hilal ya Sudan nayo pia ikafungwa mabao 2-0 dhidi ya wenyeji wao Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

**#3. Timu ya kwanza Bongo kushinda makundi**

Simba imeweka rekodi nyingine ya kuwa timu ya kwanza Tanzania kushinda ugenini hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Mara zote ambazo timu za Tanzania ikiwamo Simba yenyewe zimekuwa zikitinga hatua ya makundi, hazijawahi kushinda mechi yoyote ugenini kwenye hatua hiyo.

Yanga iliingia hatua ya makundi mwaka 1998 na haikuwahi hata kushinda mechi nyumbani, achilia mbali ugenini, Simba ambayo hii ni mara ya tatu kutinga hatua hiyo, mara mbili za nyuma, 2003 na 2018 zote hizo haikuwahi kupata ushindi ugenini.

**#4. Timu ya kwanza kushinda DR Congo**

Imeweka rekodi nyingine ya kuwa timu ya kwanza kutoka Tanzania kwenda kushinda nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Kwa miaka kadhaa timu za Tanzania zimekuwa zikipata vipigo kila zinapokwenda nchini humo.

Ikumbukwe kuwa mwaka 1978, Simba ilipata kipigo cha bao 1-0 nyumbani na ugenini na kuondolewa raundi ya pili kwenye michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Pan African nayo ilichapwa nchini DR Congo dhidi ya AS Vita ilipokwenda kucheza michuno ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 1979.


Simba ilichapwa mabao 5-0 dhidi ya AS Vita mwaka 2018, kabla ya kuchabangwa mabao 4-1 dhidi ya TP Mazembe.

**#5. Ya kwanza kushinda Nigeria**

Kwenye michuano hii hii, ilianza kuweka rekodi mapema tu ya kuwa timu ya kwanza Tanzania kushinda nchini Nigeria, ilipoifunga Plateau United bao 1-0 kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwa miaka mingi, timu za Tanzania zimekuwa zikichezea vichapo, kila zilipoenda kucheza na timu za Nigeria kama Enugu Rangers, Enyimba, na Racca Rovers.

**JE, WAJUA?**



JURGEN Klopp anakuwa kocha wa tisa Liverpool kuiongoza timu hiyo kwa jumla ya mechi 300 katika mashindano yote, lakini pia Mjerumani huyo amekuwa kocha wa kwanza kwa klabu hiyo kupoteza mechi yake ya 300 tangu Bill Shankly yalipomkuta kama hayo mwaka 1965. Liverpool ilichapwa 3-1 na Leicester City kwenye mechi ya Ligi Kuu England juzi wakati Klopp akitimiza mechi yake ya 300 kuiongoza.





## TAMISEMI yaombwa mikakati wananchi kujiunga na iCHF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeombwa kuweka mikakati ya kuhakikisha wananchi wanajiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF), ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa ugawaji wa kadi za iCHF kwa watoto 361,539 wanaoishi katika mazingira hatarishi kwenye mikoa 24 nchini, Meneja Mradi wa HPSS Tuimarishe Afya unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi, Ally Kebby, alisema mwamko wa wananchi kwasasa ni mkubwa.

Alisema ni vyema kuweka mkakati wa kuwatumia Maofisa Ugani wote waliopo kwenye Halmashauri nchini kushiriki kutoa elimu kwa wananchi ili wajiunge na mfuko huo.

"Uandikishaji unafanyika kwa kutumia TEHAMA lakini tatizo ni elimu haijafika kwa wananchi, nipongeze Shirika la Pact-Tanzania kwa kusaidia kufikia makundi maalum, kuna asilimia 26 ya Watanzania wapo kundi la watu maskini, hawa usipokuwepo mkakati mahsusi hawatafikiwa," alisema.

Alisema hatua hiyo itasaidia kufikia malengo ya serikali ya kuhakikisha kila mwananchi anajiunga na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Hata hivyo, alisema kumekuwapo na ongezeko la wananchi kuingia kwenye bima ya iCHF.

"Bima hii inawagusa wananchi wote wa Tanzania wale wenye kipato cha juu, kati na chini na hakuna bima inayoweza kuwafikia wananchi wote bila kikwazo kama iCHF," alisema.

Alisema takwimu za Novemba na Desemba mwaka jana zinaonesha mahudhurio ya zaidi ya wananchi milioni 1.5 wenye kadi za bima hiyo wametibiwa kwenye vituo vya afya nchini.

"Sisi HPSS tuahidi tutaendelea kusaidia utekelezaji wa bima hii kwa kuendelea kutoa elimu kwa sababu wananchi wengi bado hawana elimu ya kutosha," alisema.

# Mazingira biashara ya nafaka yaboreshwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imefuta na kuondoa tozo na kodi zaidi ya 250 ambazo zilikuwa kero kwa sekta binafsi ili kuweka mazingira mazuri ya kuvutia biashara hususani katika mazao ya nafaka.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, aliyesema hayo juzi katika mkutano wa wafanyabiashara wa mazao ya nafaka uliofanyika jijini hapa.

James alisema kila mwaka wizara hiyo imekuwa ikipitia kodi na kuzifanyia kazi hivyo wafanyabiashara wanatakiwa kuwazi kueleza vikwazo vyao ili serikali iboreshe.

"Wizara tunajukumu kubwa sana la kuhakikisha sehemu kubwa ya kilimo,Uvuvi na mifugo zinasonga mbele shida inakuja kweye takwimu unakuta zinatofautiana ambazo huchangia," alisema James.

**Mimi niko hapa kubeba jukumu hilo kikamilifu, tunahitaji kilimo cha nchi hii kiwe kimoja ili tuweze kupata thamani ya mnyonyoro wa mazao ya nafaka yanayolimwa nchini.**

Aliwataka wafanyabiashara kutumia mkutano huo kujadili mipango mikakati yao na suala la kodi na tozo.

"Unakuta watu wengi hawajui nini maana ya kodi na kusababisha kulalamika, ili kuondoa hilo jadili na kuuliza maswali kwa wahusika ili muondoke mkiwa na ufahamu," alisema James.

Hata hivyo, alisema Wizara hiyo na wizara nyingine haziwezi kuwakwepa wafanyabiashara.

"Hivyo nanyi kwa umoja wenu mnapaswa kusema tatizo lipo wapi ili litatuliwe na nyie msonge mbele, tunahitaji kuona kilio cha nchi kinakuwa kimoja, sote tukiungana tutafanikisha kuleta thamani ya kitu kimoja ambacho kitaleta matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla," alisema James.

Aliongeza: "Mimi niko hapa kubeba jukumu hilo kikamilifu, tunahitaji kilimo cha nchi hii kiwe kimoja ili tuweze kupata thamani ya mnyonyoro wa mazao ya nafaka yanayolimwa nchini."

Naye, Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Frank Mwega, alisema wizara hiyo ipo katika kutekeleza sera ya kukazia uchumi na mambo mengine ambayo yanaleta tija katika biashara.

Alisema dhumuni kubwa ni kutekeleza mambo muhimu ya sera ya kukazia masuala ya uchumi ambayo itawanufaisha wafanyabiashara kutokana na hivi sasa kuna masoko mengi ambayo wanahitaji kuyajua kama vile soko la Afrika, Afrika Mashariki na SADC.



Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona (TLB) Mkoa wa Dodoma, Omar Lubuva, akizungumza na wajumbe kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama hicho (hawapo pichani) juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Taasisi zaagizwa kuweka malengo kuongeza ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula, ameagiza kila taasisi ya Wizara hiyo kuhakikisha inaweka malengo ya kuongeza ajira ili serikali ifikie lengo la kutoa ajira mpya milioni nane ndani ya miaka mitano.

Aidha, ameitaka baraza la wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania kuweka mikakati ya kuhakikisha shirika hilo linajiendesha kwa faida na kuchangia uchumi wa taifa.

Dk. Chaula aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokuwa akifunga kikao cha baraza hilo lililokutana kwa ajili ya kujadili na kutathmini utendaji kazi wa shirika hilo.

"Kila mtu ndani ya Shirika ajitathmini amelifanyia nini shirika, kila taasisi imewekewa target ataongeza vipi ajira mpya za ndani kama nchi tumejiwekea ajira milioni 8,000,000 na kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 hadi 2025 imeahidi, kati ya hizo je, taasisi yako itatoa ngapi," alisema.

Aidha, alisema ni wajibu wa kila mtumishi ndani ya shirika hilo kuhakikisha anafanyakazi kwa bidii na kuongeza tija katika shirika na kuongeza uzalishaji kama ilivyokusudiwa wakati wa uanzishwaji wake.

"Nataka mjitathmini katika utendaji kazi wenu katika Mkoa yote kuhakikisha Mikoa yote inafanya vizuri na kusaidia Mikoa ambayo haifanyi kazi vizuri ili nayo ifanye kazi vizuri," alisema.

Kadhalika, alitaka wajumbe wa baraza kwenda kuyatumia mafunzo waliyoyapata juu ya huduma mpya zilizoanzishwa na shirika na kuongeza mchango katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya mawasiliano.

Awali, Posta Masta Mkuu wa Shirika hilo, Hassan Mwang'ombe, alisema baraza limekaa kwa siku tatu likishirikisha watumishi kutoka ngazi mbalimbali kwa lengo la kutathmini na kuweka malengo katika kuimarisha utendaji kazi wa shirika.





# TFS yapiga jeki vijiji ujenzi miundombinu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJIJI saba vya Kata ya Ihango katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, vimekabidhiwa msaada wa mbao 843 na Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo vyumba vya madarasa, zahanati na ofisi za vijiji.

Mbao hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na TFS kupitia shamba la miti la Kawetere ikiwa ni sehemu ya mikakati ya wasimamizi wa shamba hilo kuimarisha ushirikiano na wananchi wanaoishi kuzunguka shamba hilo ambalo ni la miti ya kupandwa.

Akiwakabidhi viongozi wa vijiji hivyo baada ya kupokea mbao hizo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema pamoja na kwamba kila kijiji kitakuwa na mahitaji yake ni vizuri viongozi hao wakaweka kipaumbele zaidi kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Ihango.

**Baada ya kukamilisha miundombinu kwenye shule ya sekondari wanaweza wakaendelea na ujenzi wa miundombinu mingine kwenye taasisi zingine zikiwamo zahanati za vijiji na ofisi.**

Alisema mbali na ujenzi wa vyumba vya madarasa pia mbao hizo zinatakiwa zitumike kutengeneza madawati ili wanafunzi wasibanane kwenye madawati machache ama kukaa chini baada ya vyumba kukamilika. Alisema baada ya kukamilisha miundombinu kwenye shule ya sekondari wanaweza wakaendelea na ujenzi wa miundombinu mingine kwenye taasisi zingine zikiwamo zahanati za vijiji na ofisi.

"Tunaushukuru sana uongozi wa shamba hili kwa ushirikiano wanaotupa, lakini wanatusaidia kutokana na ushirikiano tunaowapa kwenye ulinzi wa shamba hili, sasa nawaomba sana viongozi wa vijiji mjitahidi sana kuwaelimisha wananchi wasiharibu msitu huu," alisema Ntinika.

Aliuomba uongozi wa shamba hilo kuendelea kuvisaidia vijiji vya kata zingine nane zinazozunguka shamba hilo ili kuimarisha ulinzi kwa maelezo kuwa maeneo mengine wananchi wanaweza wakaanza kunung'unika endapo watasikia wenzao wamesaidiwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi mbao hizo, Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Kawetere, Arnold Shoo, alisema wananchi wa vijiji hivyo pamoja na vingine vinavyozunguka shamba hilo wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa kwenye ulinzi wa shamba.

Alisema wakati wa kiangazi moto umekuwa ukitokea mara kwa mara na wananchi hao wamekuwa wakishiriki kikamilifu kwenye udhibiti na hivyo kulifanya shamba liendelee kustawi.

Shoo alisema mbali na kuvisaidia vijiji hivyo mbao pia wamekuwa wakisaidia ujenzi kwa kutoa vifaa vingine zikiwamo nondo na saruji kwenye vijiji vyote vinavyozunguka shamba kulingana na mahitaji ya kila kijiji.

Vile vile, alisema wananchi wa vijiji hivyo wamekuwa wakinufaika pia na shamba hilo kwa kupata kuni za kupikia, kulima kwenye maeneo ambayo miti bado haijakua pamoja na kupata ajira za kupogolea miti kwenye shamba hilo.

"Hizi mbao zina thamani ya Sh. 5,000,000 na tunaamini zitawasaidia wananchi hao, lakini hatutaishia hapa bali tutaendelea na kwenye vijiji vingine, lakini pia kuna miti ambayo sisi tumeotesha na tunagawa bure kwa wananchi wa vijiji hivi pamoja na taasisi za Serikali zinazohitaji," alisema Shoo.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Ihango, Haustin Kwimbe, alisema msaada huo utasaidia kumaliza matatizo ya vijiji vya kata yake na kwamba gharama hizo zilitakiwa zibebwe na wananchi wake pamoja na Halmashauri.

Alisema mbali na mbao hizo pia bado wana mahitaji mengine, hivyo akawaomba wadau wengine wa maendeleo mkoani Mbeya kusaidia kupata mahitaji hayo ili kumaliza matatizo ya wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (kushoto), akimshukuru Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti la Kawetere, ambalo linasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Arnold Shoo, baada ya kukabidhiwa mbao 843 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwenye vijiji saba vya Kata ya Ihango mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wadau wataka bodi ya mpunga

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WADAU wa kilimo cha mpunga wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameiomba Serikali kuunda bodi ya zao hilo ambayo itasaidia kuliendeleza na kukabiliana na matatizo yanayolikabili ikiwamo kupanga bei inayoendana na gharama za uzalishaji.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wa kikao cha kujadili mpango wa uboreshaji wa Mnyororo wa thamani ya zao la mpunga kilichofanyika wilayani Mbarali.

Christina Mwakaganda, Mwenyekiti wa kikundi cha wakulima wa mpunga wa Kijiji cha Madabaga wilayani Mbarali alisema baadhi ya mazao nchini yana bodi ambazo zimeundwa kwa ajili ya kushughulikia matatizo yanayoyakabili lakini kwenye mpunga haipo.

Alisema kazi ya bodi hizo huwa ni pamoja na kupanga bei elekezi ya zao husika kulingana na soko la kimataifa pamoja na gharama za uzalishaji, lakini kwenye mpunga hakuna kitu kama hicho hali ambayo inalifanya zao hilo kukosa udhibiti.

Alisema bei ya mpunga imekuwa ikibadilika mara kwa mara kutokana na kuuzwa kwa makubaliano kati ya wanunuzi na wakulima hali ambayo alidai wakati mwingine bei huwa haiendani na gharama za uzalishaji.

"Kwenye mazao kama korosho, kahawa, tumbaku na hata pamba kuna bodi maalumu ambazo ndizo zinasimamia biashara ya mazao hayo, sasa na sisi wazalishaji wa mpunga tunaiomba Serikali itusaidie tuwe na bodi yetu ili iwe rahisi kushughulikia matatizo yetu," alisema Mwakaganda.

Mwenyekiti wa Baraza la Mchele nchini, Winnie Bashagi, alisema Tanzania ina maeneo mengi ambayo yanafaa kwa kilimo cha mpunga lakini hayajatumika ipasavyo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo teknolojia.

Alisema eneo linalofaa kwa kilimo nchini ni hekta milioni 21, lakini linalotumika mpaka sasa ni chini ya asilimia 10, hivyo akasisitiza kuwa endapo itaundwa Bodi ni rahisi hata kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji.

"Endapo tungekuwa na uwezo wa kulima eneo lote linalofaa, kuna uwezekano mkubwa mpaka sasa tungekuwa tunalisha watu wote wa Bara la Afrika na pengine hata mabara mengine tungekuwa tunawapelekea," alisema Winnie.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti nchini ya REPOA, Godfrey Kalaghe, alisema unahitajika utafiti wa kina kuhusu kilimo cha Mpunga kabla ya kuwashauri watunga sera kufanya maamuzi ya aina yoyote.

# Watendaji waengua mawakala ukusanyaji wa kodi Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imeanza kukusanya mapato ya ndani kwa kutumia maofisa watendaji wa kata badala ya kuwatumia mawakala ili kupunguza gharama za ukusanyaji na kuongeza kasi ya utekelezaji wa utekelezaji wa miradi.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kivuma Msangi, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema walikuwa wanalazimika kuwalipa mawakala asilimia 20 ya mapato waliyokuwa wanakusanya.

Alisema walifanya majaribio ya kukusanya mapato hayo kwa kutumia watendaji kwenye kata za Imalio-Songwe na Madibira wakabaini kuwa kuna ufanisi mkubwa na ndio maana wameamua kutumia utaratibu huo kwenye Wilaya nzima.

Alisema wakati wanafanya majaribbio hayo walibaini kuwa asilimia 20 ya mapato waliyokuwa wanawalipa mawakala ni fedha nyingi ambazo wakiziokoa zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema Halmashauri hiyo inakusudia kutumia zaidi ya Sh. Bilioni 45 kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambazo zitatoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato zikiwamo za kutoka Serikali Kuu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## NAFASI ZA KAZI

**WANAHITAJIKA**
**SECRETARY MZOEFU MWENYE CUSTOMER CARE.**

**SIFA:**
**UMRI** – MIAKA 25 HADI 35
**ELIMU** - KIDATO CHA NNE AU CHA SITA
UZOEFU WA KAZI - MIAKA MIWILI NA KUENDELEA
NAMBA YETU YA SIMU NI: **0787 207 369.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABRAHAM FRANK MARO** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **S.0322/0060** kilichotolewa na **KOLILA HIGH SCHOOL** mwaka **2007.** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0133/0635** kilichotolewa na **MINAKI HIGH SCHOOL** mwaka **2010.** University Certificate namba **K 19 0004** kilichotolewa na **KILIMANJARO MEDICAL UNIVERSITY COLLEGE (KCMUCO)** mwaka **2015.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. **Taarifa ya Polisi: SHI/KAH/RB/879590/2020.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 53/2019**
**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA YA LINDI JINAI NA. 76/2018**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA -----MRUFANI**
**DHIDI YA**
**JUMA ALLY HAMIS @ MKULUPALILE ------MJIBU RUFANI**
**KWA:**
**JUMA LLY HAMISI @MKUKUPALILE**
**MAKONGORO**
**LINDI**

**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUDIKA MBELE YA MAHAKAMA KUUU YA MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 19/02/2021 SAA 2;30 ASUBUHI BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 8/2/2021.

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 33/2019**
**MKURUGENZI MASHTAKA .......................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**SALUM ABDALLAH @NALIOGO**
**ADAMU SAIDIA @OHIMBA ...........WAJIBU RUFAA**
**KWA**

1. **SALUM ABDALLLAH @NALIOGO**
   **MADIGO**
   **LINDI**
2. **ADAMU SAIDI @OHIMBA**
   **MADIGO**
   **NYANGAMALA**
   **LINDI**

**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUDIKA MBELE YA MAHAKAMA KUUU YA MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 19/02/2021 SAA 2;30 ASUBUHI BILA KUKOSA.
KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA, BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO.
IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 8/2/2021.

**A.H. MSUMI**
**NAIBU MSAJILI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

## JAH PEOPLE INVESTMENT TRANSPORT CO. LTD

## JOB VACANCIES

I .ACCOUNT OFFICER
ACCOUNTING
1.VAT filling and reconciliation
2.Tax laws and regulations compliancy
3.Cash and petty cash controlling
4.Financial accounting knowledge
5.Accounting books handling
6.To perfom any other duties assigned by supervisors

At least two years working experience from any recognized institute
Bachelor degree in / of accounts from any recognized university
**CPA- holder given advantage**

II. TRUCK DRIVERS
TANZANIAN AGED BETWEEN 20 TO 50 YEARS
AT LEAST TWO YEARS EXPERIENCE IN DRIVING HEAVY DUTY TRUCKS
HOLDER OF VALID DRIVING LICENCE

FROM THE ANNONCEMENT DATE TO 23RD FEB, 2021
25TH FEB, 2021 TIME 08:00 AM AT JAHPEOPLE YARD MAKAMBAKO.
All application should be send through
email; jahpeoples@yahoo.com
OR
MANAGER
JAH PEOPLE INVESTMENT CO LTD
P.O.BOX 190,
MAKAMBAKO, NJOMBE TANZANIA.

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Seneti yamwondolea mashtaka Trump

**Washington, MAREKANI**

BARAZA la Seneti nchini Marekani, limemwondolea mashtaka Donald Trump.

Mashtaka hayo yalihusu kuchochea maasi na uvamizi wa bunge baada ya Trump kushindwa katika uchaguzi.

Maseneta 57 walipiga kura ya kumtia hatiani rais huyo mstaafu wa Marekani wakiyakataa mashtaka dhidi yake.

Wajumbe saba wa chama cha Republican, waliungana na wajumbe wa Chama cha Democratic, kumtia hatiani Trump, ingawa idadi hiyo haikufikia theluthi mbili iliyohitajika.

Kiongozi wa maseneta wa Chama cha Republican, Mitch McConell, alisema kwamba Donald Trump alihusika na kuchochea mashambulio kwenye bunge, hata hivyo hakupiga kura ya kumtia hatiani rais huyo.

McConell alisema kikatiba, Trump hastahili kushtakiwa kwa sababu sasa hayupo madarakani.

Matokeo ya Trump kuondolewa mashtaka, kulisababisha migawanyiko ya utata nchini Marekani kisiasa na kusababisha maasi dhidi ya mhimili wa demokrasia, bunge.

Akizungumza baada ya hukumu hiyo kutolewa, Rais Joe Biden alisema kipindi hiki katika historia ya Marekani kinakumbusha kwamba demokrasia ni jambo nyeti.

Rais Biden alisema ingawa Trump hakutiwa hatiani, kiini cha mashtaka hakiwezi kukanushwa.

DW




Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Huawei, Ren Zhengfei, mwishoni mwa wiki aliwaambia waandishi wa habari, kampuni hiyo itazingatia utandawazi, sera za wazi kwa maslahi ya kampuni na uchumi. **PICHA/ HUAWEI**

# Tunisia yaokoa mashua ya wahamiaji haramu

**Lampedusa, ITALIA**

JESHI la Wanamaji la Tunisia, lamewaokoa wahamiaji haramu 25.

Wahamiaji hao waliokolewa kutoka kisiwa cha Kaskazini Magharibi cha Lampedusa.

Katika taarifa iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi, ilitangazwa kuwa kulikuwa na wanawake sita, kati ya wahamiaji hao wenye asili ya Kiafrika waliokolewa na mwili wa mmoja wa wahamiaji ulitolewa baharini.

Hii ni baada ya mashua iliyokuwa imewabeba kuzama.

Iliripotiwa kuwa shughuli za uokoaji zilifanywa kwa uratibu kati ya Kituo cha Utafutaji na Uokoaji cha Jeshi la Wanamaji la Tunisia, Kaskazini Magharibi mwa Kisiwa cha Lampedusa cha Italia na vituo vya Utafutaji na Uokoaji Roma na Malta.

Kulingana na habari kutoka kwa wahamiaji waliookolewa, ilibainika kuwa wahamiaji hao waliondoka mwishoni mwa wiki ufukwe wa Sidi Mansur katika jiji la Safaks, Kusini mwa mji mkuu wa Tunisia.

TRT

# Huawei yasisitiza kuendeleza utandawazi

**Taiyuan, CHINA**

KAMPUNI ya Huawei imeahidi kuzingatia mkakati wake wa utandawazi, licha ya shinikizo la nje.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Ren Zhengfei alitoa wito huo, akilenga utawala mpya wa Marekani, kuja na sera za wazi kwa maslahi ya kampuni na uchumi.

Kauli hiyo ni ya kwanza kutolewa na mwanzilishi wa hiyo, tangu mabadiliko ya utawala wa Marekani.

Zhengfei aliyasema hayo akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari, Taiyuan mji mkuu wa Mkoa wa Kaskazini mwa China, Shanxi, baada ya kuzindua maabara ya ubunifu wa madini.

"Biashara inanufaisha pande zote mbili. Kuruhusu kampuni za Marekani kusambaza bidhaa kwa wateja wa China. Ikiwa uwezo wa uzalishaji wa Huawei utakua, kampuni za Marekani zitauza zaidi.

Sote tutanufaika. Ninaamini utawala mpya utapima maslahi haya wakizingatia sera zao," alisema Zhengfei.

Alisema, Huawei inajenga thamani, ekolojia na uchumi mpana na kwamba kampuni hiyo imeunda mitandao ya 5G katika miji ya Ulaya,

Zhengfei alitaja maeneo mengine kuwa ni Asia na Mashariki ya Kati, huku majaribio ya mtandao huo yakiwa na ufanisi.

"Ukweli watumiaji wa hali ya juu wanaweza kutumia iPhone 12 kikamilifu kwenye mitandao yetu ya 5G, huko Ulaya ni ushahidi wa ubora wa mitandao yetu," alisema Zhengfei na kuongeza...

"Kama binadamu tunavyoendelea kufanya maendeleo, hakuna kampuni inayoweza kukuza tasnia ya utandawazi peke yake. Tunahitaji juhudi za pamoja duniani kote."

Serikali ya Marekani imekuwa ikifanya kampeni dhidi ya Huawei, miaka miwili iliyopita ikidai vifaa vya Huawei vinaweza kutumiwa kupeleleza Wamarekani, bila kuwasilisha ushahidi wowote.

Huawei alikataa mara kwa mara madai hayo na nchi zingine chache zilikubali shinikizo la Marekani.

Zhengfei alisema uhai wa Huawei uko juu kuliko awali.

"Tumepata njia mpya zaidi za kushinda changamoto zetu. Mapato na mauzo yetu mwaka 2020 yalikuwa makubwa kuliko miaka iliyopita," Zhengfei aliwaambia waandishi wa habari.

Zhengfei alisema matokeo ya biashara ya Huawei kwa miezi tisa ya kwanza ya mwaka jana, yalionyesha mapato yalikuwa jumla ya Yuan bilioni 671.3 sawa na Dola 98.57 bilioni, ongezeko likiwa asilimia 9.9 ikilingaishwa na mwaka 2019.

"Tutaendelea kuwahudumia wateja wetu vizuri kwa kuwajengea thamani zaidi. Tunataka wawe na imani ya kudumu ndani yetu na tunatumai kuwa hawatayumba kwa sababu ya shinikizo la kisiasa, " alihitimisha Zhengfei.



# MESSI

## AIFIKIA REKODI YA XAVI BARCELONA

**BARCELONA, Hspania**

LIONEL Messi ameifikia rekodi ya Xavi ya kuichezea Barcelona mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kushuka dimbani kwenye mchezo dhidi ya Deportivo Alaves, Jumamosi.

Ilidhaniwa kwamba, kocha Ronald Koeman angemuacha nje Messi kwenye mchezo huo kwa ajili ya kujiandaa na ule wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho Jumanne dhidi ya Paris Saint-Germain hatua ya 16-bora.

Hata hivyo, Koeman akaamua kumjumuisha nahodha huyo kwenye kikosi hicho kilichoibuka na ushindi wa mabao 5-1.

Messi alifikisha mechi 505 alizoichezea Barcelona kwenye Barca, na kuifikia rekodi hiyo iliyowekwa na Xavi.

Na sasa raia huyo wa Argentina ana nafasi ya kuweka rekodi yake kwenye mchezo ujao wa LaLiga dhidi ya Cadiz utakaopigwa mwishoni mwa wiki hii nyumbani.

## KLOPP AKATA TAMAA UBINGWA LIVER EPL

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amekiri Liverpool haina matumaini ya kutetea taji la Ligi Kuu England (EPL), msimu huu baada ya kukubali kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Leicester City, juzi Jumamosi.

Mohamed Salah alianza kwa kuifungia Liverpool pale kwenye dimba la King Power, lakini 'Wekundu' hao wakajikuta wakiruhusu mabao matatu ndani ya dakika saba.

Matokeo hayo yanamaanisha Liverpool imepoteza mechi tatu za ligi mfululizo kwa mara ya kwanza tangu Novemba 2014 wakati kocha wa sasa wa Leicester, Brendan Rodgers alipokuwa kocha wao na wakabiliwa na wakati mgumu wa kumaliza kwenye nne bora.

Klopp hakuwa na furaha na uamuzi wa VAR kuwapa Leicester bao la kusawazisha, baada ya James Maddison awali kuonekana kwamba aliotea kabla ya kupiga shuti lililojaa wavuni.

"Sidhani kama tunaweza kupunguza pengo hili mwaka huu kiukweli," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari ambapo mchezo huo ulikuwa ni wa 300 tangu aanze kuifundisha Liverpool.

"Tunatakiwa kushinda mechi na nafasi kubwa ilikuwa leo (juzi), mchezo ulikuwa mzuri sana. Tunatakiwa kushinda kila mchezo. Tunatakiwa kuepuka makosa.

"Kila kitu kipo mikononi mwetu, bila shaka hatuwezi kuepuka maamuzi ya VAR, lakini mambo mengine yote yapo mikononi mwetu.

"Leo (juzi) hatukufanya kile tulichopaswa kufanya na ndio maana wakafunga mabao mawili ya haraka. Kwa uhakika kabisa tuna nafasi ngumu."

Liverpool sasa imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara 32 katika mechi 24 za ligi hadi sasa.

## PIOLI ABARIKI KICHAPO MILAN

**MILAN, Italia**

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, anatambua "hakuna kilichofanya kazi" wakati timu yake ikikumbana na kipigo cha kwanza ugenini kwenye Serie A tangu Desemba 2019 dhidi ya Spezia, Jumamosi.

Rossoneri hao walikuwa kwenye wakati mgumu pale katika dimba la Alberto Picco na walishindwa kupiga shuti hata moja lililolenga goli kwa mara ya kwanza tangu Agosti 2019, wakati mabao ya Giulio Maggiore na Simone Bastoni yakawafanya waondoke dimbani kichwa chini kwa kichapo cha 2-0.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Milan kupoteza mchezo dhidi ya timu illiyopanda daraja, nyumbani kwao tangu ilipochakwa na Benevento, Aprili 2018.

Matokeo hayo yanamaanisha kwamba, Inter Milan ambao watacheza na Milan wiki hii - wanaweza kuwapiku wapinzani wao hao wa jiji moja, kama jana Jumapili walishinda dhidi ya Lazio.

Milan sasa imepoteza mara tatu kwenye Ligi Kuu msimu huu na Pioli amesema hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza walistahili kichapo hicho.

"Litakuwa somo zuri kwetu sote; tutaelewa kwamba tusipocheza vizuri kwa kiwango fulani, tutanyanyaswa kama hivi," alisema akiiambia DAZN.

"Spezia walistahili ushindi. Hiki ni kichapo cha kwanza tulichostahili msimu huu, hatukuwa na ubora wa kutosha au nguvu na wapinzani wetu walitumia vizuri udhaifu wetu.

"Sisi ni timu ambayo hatupaswi kushinda vibaya. Mara zote tunajaribu kucheza kwa kasi na kwa nguvu kubwa, lakini leo tulistahili kufungwa."



HABARI MICHEZO



# SPURS

## IMEPOTEZA KIBINGWA - MOURINHO

**MANCHESTER, England**

JOSE Mourinho hakushangazwa kuona "timu iliyochoka sana" ikifungwa na Manchester City, ingawa anahisi kwamba Tottenham ilikuwa kwenye mchezo kabla ya kuadhibiwa kwa "penalti ya kisasa".

Spurs imeshinda mara moja katika mechi sita za mashindano yote baada ya kuchezea kichapo cha 3-0 kutoka kwa City kwenye Ligi Kuu, ikiwa ni siku tatu tu kutoka itolewe kwenye FA na Everton.

Tottenham imeruhusu mabao nane wiki hii, matano yakiwa pale katika dimba la Goodison Park, ikiwa ni michezo miwili mibaya zaidi tangu Mourinho aanze kazi ya ukocha.

Licha ya kuwa na mashuti saba katika lango la City waliokuwa na mashuti 15 na matatu tu yakilenga goli - yote yalipatikana kipindi cha pili na kocha huyo wa Spurs aliridhika na kiwango cha timu yake.

Tottenham walikuwa na nafasi nzuri wakati shuti la Harry Kane lilipogonga mwamba, lakini faulo ya Pierre-Emile Hojbjerg kwa Ilkay Gundogan ikazaa penalti iliyofungwa na Rodri.

Baadaye Gundogan akafunga mara mbili na kuiwezesha City kuibuka na ushindi huo mnono.

"Ni timu iliyokuwa fiti dhidi ya timu iliyochoka sana, lakini timu yangu ilianza mchezo vizuri sana na ilitawala," alisema Mourinho akiiambia Sky Sports.

"Lakini baada ya 'penalti ya kisasa' - walituweka kwenye wakati mgumu na tukapoteza mchezo.

"Lakini nina furaha kubwa na mtazamo wa wachezaji wangu walivyocheza. Nilikuwa na watu uwanjani waliojituma kweli kweli kwa kujaribu kufanya kila kitu."

# Milan wamtaka jumla Diaz

**MILAN, Italia**

KLABU ya AC Milan inataka kumsajili moja kwa moja mshambuliaji wa Real Madrid, Brahim Diaz ambaye anacheza kwa mkopo pale San Siro, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, kuonyesha kiwango bora.

Vyanzo vinaeleza kwamba mabosi wa Milan wanania ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu, ingawa bado hawajafanya mazungumzo na Real Madrid.

Wakati Brahim mara nyingi amekuwa akitaka kufanikiwa ndani ya Bernabeu, Madrid wataangalia kama watataka kumbakiza au kumuuza baada ya kumalizika kwa msimu wa 2020-21.

Kutokana na kutua Milan kwa mkopo Septemba 2020, Brahim amekuwa mwepesi na kuyazoea haraka maisha ya Italia na amekuwa ni mchezaji muhimu katika kikosi cha kwanza cha Pioli.

Amecheza mechi 25 katika mashindano yote, amefunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho mbili ingawa aliikosa michezo miwili iliyopita ya Milan kutokana kuwa na majeruhi.

Milan wameijulisha familia ya Diaz kwamba, wanampango wa kufanya dili la kudumu na mchezaji huyo ambao Madrid wanataka kiasi cha euro milioni 30 ili kumuachia.

Diaz alijiunga na Madrid akitokea klabu ya Manchester City Januari 2019 ingawa alikuwa akitumika kama mchezaji wa akiba kwa misimu yake miwili ndani ya klabu na kucheza mechi 21 pekee kwa ujumla.




# PSG ipo tayari kuivaa Barcelona - Pochettino


**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino amesema Paris Saint-Germain itakuwa tayari kuivaa Barcelona kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kesho, Jumanne.

PSG itasafiri kwenda kwa Barca ya Lionel Messi kesho Jumanne kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 utakaopigwa pale Camp Nou baada ya Jumamosi kuichapa Nice mabao 2-1 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Mabao kutoka kwa Julian Draxler na Moise Kean yakaiwezesha PSG kupata ushindi huo dhidi ya Nice pale kwenye mji mkuu wa Ufaransa, ambapo sasa mabingwa hao wa Ligue 1 wameendeleza ushindi wa mechi nne kwenye mashindano yote.

Mara baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu Pochettino alizungumzia umuhimu wa ushindi huo kuelekea mchezo dhidi ya Barcelona, lakini anaamini PSG



watakua tayari.

"Tunatakiwa kuwa tayari (dhidi ya Barcelona)," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa sababu tuna mchezo muhimu Jumanne. Na timu itakuwa tayari kwa ajili ya mchezo huu.

"Kitu cha kwanza kitakuwa timu kuamka, kinguvu na akili (kabla ya kuivaa Barcelona). ni muhimu kuchaji betrii.

"Kwa upande wa mbinu, tutafanya kazi kubwa uwanjani kuhakikisha kwamba tunakuwa kwenye kiwango bora.

"Ni kitu ambacho tumekuwa tukijiandaa kwa wiki kadhaa, hivyo wachezaji wanaweza kutekeleza mpango wa mchezo huu."

PSG imeshinda mechi zake sita kati ya nane za Ligue 1 chini ya Pochettino (sare moja, imepoteza moja), baada ya kushinda mechi tatu kati ya saba zilizopita mwishoni mwa mwaka 2020 (sare mbili, imepoteza mbili).

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: LIVER BADO INAWEZA KUTWAA EPL

●●●Ni ile ile niliyokutana nayo mwaka jana, ubora walioonyesha na kile walichofanya dhidi ya...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaamini Liverpool bado wanaweza kutetea kombe lao la Ligi Kuu England, EPL, licha ya kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kuonekana kulikatia tamaa taji hilo.

City inaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi saba, na 13 ikiizidi Liverpool, huku wakiwa na mchezo mmoja mkononi baada ya juzi Jumamosi kuibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Tottenham.

Kocha wa Liverpool, Klopp amekiri kwamba, hawana matuaini ya kutetea taji hilo msimu huu baada ya kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Leicester City.

Lakini Guardiola aliwaambia waandishi wa habari: "Kwa kile nilichokiona, kwa namna walivyocheza dhidi ya Leicester, bila shaka tukipoteza mchezo wao wanaweza kufanya makubwa.

"Ni Liverpool ile ile niliyokutana nayo mwaka jana, lakini kwa sasa umaliziaji wao bado si bora sana kama ulivyokuwa mwanzo. "Ubora walioonyesha na kile walichofanya dhidi ya Leicester, wanaweza kufanya jambo fulani mbeleni.

"Soka la kisasa ukiwa ndani ya boksi ni rahisi kufunga na kutengeneza mashambulizi, lakini wao naona kuna kitu fulani wanakikosa kwa sasa. Lakini soka ni mbinu, kuna wakati unazidiwa na kuna wakati unakuwa kwenye ubora wako.

"Ubora wa timu yao bado uko pale pale. Sidhani kama wamepoteza ubora wao wa kusukumiza mipira mbele au kucheza, mara zote wanatengeneza nafasi nyingi kuliko wapizani wao.

"Huwa sipendi kupata shida nikicheza nao, lakini mara zote napenda kuwaangalia Liverpool wakiwa dimbani."

City imebakia kuwa timu ambayo haijafungwa katika mechi 23 zilizopita kwenye mashindano yote (ikishinda 20 na kutoka sare tatu), ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara sita na Manchester imeendeleza rekodi yao ya kushinda dhidi ya timu kubwa kwenye mashindano yote kwa mechi 16.

## KWA UFUPI

**ARSENAL YAMKOMALIA BALOGUN**

ARSENAL haijakata tamaa ya kushawishi kumpa mkataba mpya nyota wake, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 19 raia wa England. ***(Sun)***

**UTD YAJIPANGA KWA KOUNDE**

MLINZI wa Sevilla, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, amewekwa kipaumbele cha Manchester United kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto, baada ya Bayern Munich kumnasa mlinzi wa kati, Dayot Upamecano, mwenye umri wa miaka 22, kutoka RB Leipzig. ***(Express)***

**TUCHEL AONYA VIJANA CHELSEA**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amewaonya wachezaji vijana wa timu hiyo atawatoa kwa mkopo ili wakajiimarisha zaidi kwa uchezaji. ***(Goal)***

**LIVERPOO YAMTAKA BREMER**

LIVERPOOL imemfanya mlinzi wa kati wa Torino na Brazil, Bremer mwenye umri wa miaka 23, kama ndio chaguo lao la kwanza kwenye usajili ujao wa kipindi cha majira ya joto. Mchezaji huyo thamani yake ni pauni milioni 10. ***(Mirror)***

**NEUHAUS AGEUKA LULU**

LIVERPOOL, Manchester City, Juventus na Bayern Munich zinamfuatilia kiungo wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Florian Neuhaus mwenye umri wa miaka 23. ***(90 min)***

**TAPIA AWINDWA ULAYA**

KLABU za Atletico Madrid, Juventus na Paris St-Germain ni miongoni mwa klabu za Ulaya zinazomuwania kiungo wa Celta Vigo na Peru, Renato Tapia mwenye umri wa miaka 25. ***(AS)***

**SOLSKAJAER AKOMAA NA HAALAND**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amebainisha kwamba, "anamfuatilia" straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland raia wa Norway mwenye umri wa miaka 20, baada ya kushindwa kumsajili mwaka jana. ***(MEN)***

**WENGER AMTAJA VARDY ARSENAL**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, amesema alijaribu kila njia kutaka kumsajili straika, Jamie Vardy mwenye umri wa miaka 34, kutoka Leicester City mwaka 2016. ***(beIN Sport, via Star)***

**BRADY AWANIWA CELTIC**

KIUNGO wa Burnley raia wa Ireland, Robbie Brady mwenye umri wa miaka 29, anawaniwa na Celtic. ***(Mirror)***

**ZIYECH KUONDOKA CHELSEA**

WINGA wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 27 raia wa Morocco, anafikiria kuhusu majaliwa yake, baada ya kukosa namba kwenye kikosi hicho tangu alipohamia hapo akitokea Ajax. ***(Corriere Dello Sport)***

**RAPHINHA KUTUA UNITED**

MANCHESTER United inaweza kuwaunganisha kiungo wa Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26, na mchezaji mwenzake wa zamani wa Sporting Lisbon, Raphinha. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 raia wa Brazil alijiunga na Leeds United kipindi cha majira ya joto kilichopita. ***(MEN)***

HABARI MICHEZO

# ZANZIBAR MWENYEJI MICHUANO CONIFA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ZANZIBAR imepewa uenyeji wa michuano ya Afrika kuwania kombe la nchi zisizo wanachama wa moja kwa moja wa Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na Fifa (CONIFA AFRIKA) inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Mei mwaka huu visiwani hapa, imeelezwa. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) na kutiwa saini na Rais wa shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu, imeeleza kuwa mashindano hayo yatashirikisha nchi za Afrika ambazo ni wanachama wa CONIFA.

Taarifa hiyo ilieleza kupitia mashindano hayo ya CONIFA Afrika timu itakayoibuka bingwa itafuzu kucheza mashindano ya Kombe la Dunia ya CONIFA mwaka 2022.

Mashindano hayo ya CONIFA Afrika yatashirikisha Jumla ya nchi 10 ambazo ni mwenyeji Zanzibar, Barotseland (Zambia), Matebeleland (Zimbabwe), Sahara ya Magharibi (Western Sahara), Kabylia (Algeria), Yorubaland (Nigeria), Biafra (Nigeria), Barawa (Somalia), Somaliland, Visiwa vya Chagos (Mauritius) na Lesotho. Aidha, taarifa hiyo ilisema kuwa kupitia mashindano hayo timu zinazoshiriki zitapata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali vya Utalii vilivyopo hapa nchini.

Zanzibar iliwahi kushiriki michuano ya Kombe la Dunia ya CONIFA mwaka 2012 hukoKurdistan kusini mwa Asia.

# Mkwasa atoa sababu kipigo Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kipigo cha mabao 2-0 ilichokipata Ruvu Shooting kwenye uwanja wake wa nyumbani, Mabatini Mlandizi mkoani Pwani dhidi ya Ihefu FC, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Mkwasa, amesema kusimama kwa Ligi Kuu kumechangia kwa kiasi kikubwa timu yake kufungwa.

Ijumaa iliyopita, Ruvu Shooting ilikumbana na kipigo hicho, baada ya kufanya vizuri kwenye mechi nyingi kabla ya Ligi Kuu kusimama kupisha mechi za Kombe la Mapinduzi na Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

"Ni kweli nimepoteza, lakini unajua kusimama kwa ligi nako kumechangia sana kipigo hiki kwa sababu wachezaji wamekaa muda mrefu bila kucheza. Kwanza niliwaruhusu wachezaji wangu wakapumzike, halafu baada ya kurejea hatukuwa na mechi za kujipima nguvu, lakini nadhani taratibu tu watakaa sawa," alisema Mkwasa.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila, mbali na kuwasifu vijana wake kwa ushindi, alisema pamoja na ufundi wake, lakini usajili wa dirisha dogo nao umechangia kwa kiasi kikubwa kuifanya timu kuwa imara.

"Haikuwa mechi rahisi. Na hata tulipotoka nyumbani niliwaambia vijana wangu kuwa tunakwenda kucheza mechi ambayo haitokuwa rahisi kama wanavyofikiri na wanachotakiwa ni kupambana," alisema Katwila, kocha wa zamani wa Mtibwa Sugar.

Kwa matokeo hayo, Ihefu inakwea hadi nafasi ya 16, ikiwa na pointi 16, huku Ruvu Shooting ikiwa kwenye nafasi ya tano kwa pointi zake 28.

WAMEKAA...




Deus Kaseke akishangilia baada ya kutokea benchi na kuifungia Yanga bao la kuongoza dakika ya 86, kabla ya Pastory Athanas kuisawazishia Mbeya City kwa mkwaju wa penalti dakika ya 90, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. Pembeni ni Tuisila Kisinda. **MPIGAPICHA WETU**

# KMC yataja uwanja chanzo kipigo Prisons

**Na Mwandishi Wetu**

UWANJA wa Nelson Mandela ni miongoni mwa kikwazo kwa KMC FC kushindwa kupata matokeo kwenye mechi yao ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons Ijumaa iliyopita, umeeleza uongozi wa klabu hiyo.

KMC ambayo ilikubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa wenyeji wao hao, imesema walishinda kuibuka na ushindi kutokana na kufanya mazoezi uwanja ukiwa umejaa maji jambo lililowapa ugumu kupata matokeo.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alimwambia mwandishi wetu kuwa walishindwa kupata pointi tatu kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki kwao licha ya ubora wa kikosi chao.

> **"Tukiwa ugenini hatukupata ushindi ipo wazi licha ya kwamba kikosi chetu ni imara na kinacheza kwa kujiamini, ila hatujakata tamaa sasa tunajipanga dhidi ya Mwadui FC, Februari 16.**

"Uwanja haukuwa mzuri, tangu tumefika mvua zilikuwa zinanyesha na ulikuwa umejaa maji jambo ambalo lilifanya wachezaji washindwe kuonyesha kiwango kizuri, wapinzani wetu wamepata nafasi na wamezitumia hivyo wanastahili pongezi," alisema.

# Morocco: Sakata Namungo ni somo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kukutana na mazito nchini Angola, Kocha Mkuu wa Klabu ya Namungo, Hemed Morocco, amesema mambo yaliyowakuta ni sehemu ya mchezo jambo ambalo linawafanya wajue namna ya kujipanga wakati ujao.

Ijumaa Namungu ilianza safari kuelekea Angola kwa ajili ya mechi yao ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CD de Agosto ya nchini humo, lakini ikajikuta ikizuiwa Uwanja wa Ndenge wa Luanda Februari 13 kwa kile kilichoelezwa kuwa wachezaji wao watatu pamoja na kiongozi mmoja kukutwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) pamoja na serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje waliweka nguvu katika kufuatilia sakata hilo ambapo majibu yalitolewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwamba mchezo wao ambao ulipaswa kuchezwa jana, Jumapili umefutwa hadi hapo kamati husika itakapotolea uamuzi. Lakini Morocco alimwambia mwandishi wetu kuwa wanamshukuru Mungu wapo salama ila yaliyotokea ni somo kwao.

"Hii ni changamoto kwetu na ni somo pia, hivyo hatuna la kusema kwa sasa, tunarejea kujipanga kwa ajili ya mechi zetu zijazo," alisema kabla ya timu hiyo kutua nchini jana.

# Michezo

Jumatatu Februari 15, 2021

Nipashe



## GUARDIOLA: LIVER BADO INAWEZA KUTWAA EPL

HABARI UK 22

**MMETUKUNA SANA...**



Mashabiki wa Simba wakiwa wamejitokeza kwa wingi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kuipokea timu hiyo ikitokea DR Congo, licha ya awali kutangaziwa wasijitokeze kwenda kuilaki hadi timu hiyo itakapofanya makubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Simba ilishinda bao 1-0 dhidi ya AS Vita Ijumaa iliyopita. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAREJEA NA UJUMBE MZITO CAF

●●●Huku ikieleza siri ya ushindi, yasema kamwe haitabweteka mpaka kieleweke, kuifuata Biashara United kesho...

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa nchi kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, ambao itapendeza zaidi kwa kuwaita timu yenye jukumu la kuitangaza nembo ya Afrika Mashariki na Kati katika michuano hiyo, wamereja nchini wakitokea DR Congo wakiwa na ujumbe mzito wa kufanikiwa kushinda mechi yao ya kwanza ya hatua ya makundi dhidi ya AS Vita.

Simba ambayo ni timu pekee kutoka Afrika Mashariki na Kati iliyofanikiwa kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya AS Vita Ijumaa iliyopita na juzi ililala Addis Ababa, Ethiopia kabla ya jana kutua jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema wamefurahi kupata ushindi huo katika mechi ya kwanza ugenini, lakini pia wamejifunza mengi katika michuano hiyo.

Alisema wamejifuza siri kubwa ya kuweza kupata mafanikio katika michuano hiyo ni kuwekeza zaidi katika uchambuzi wa mchezo husika ili kuwajua vema wapinzani wao na kutoa motisha kwa wachezaji.

"Kwanza tumejifunza lazima tuwekeza katika 'analysis' (uchambuzi) kuweza kujua wapinzani ili kupata akili zaidi ya kuwapiga wakiwa uwanjani na motisha zaidi kwa wachezaji," alisema.

Aidha, alisema wanashukuru kwa matokeo walioyapata kwa kuwa wameipeperusha vema bendera ya Tanzania wakiwa wamevaa jezi zenye ujumbe wa "Visit Tanzania" kwa mara ya kwanza.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema matokeo hayo yanawapa nguvu ya kufanya vizuri zaidi, lakini kamwe hayatawapa kiburi kwamba tayari wana uhakika wa kufuzu robo fainali na badala yake akili yao wanaielekeza katika kushinda mechi zijazo.

"Akili yetu isituelekeze huko, bado tuna kazi ngumu ya kufanya ili kuweza kupata pointi zitakazotuvusha robo fainali, hivyo kamwe hatutabweteka hadi tutakapojihakikishia kutinga robo fainali," Manara alisema.

Alisema wachezaji wataelekea moja kwa moja kambini na jioni watafanya mazoezini na kisha baadaye watapewa mapumziko ya usiku mmoja kabla leo mchana kurejea kufanya mazoezi na maandalizi ya safari yao ya kesho, Jumanne kwenda Musoma wakipitia Mwanza tayari kwa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United itakayopigwa Alhamisi wiki hii. "Baada ya mechi hiyo tutarejea Dar es Salaam tayari kwa maandalizi ya mechi dhidi ya Al Ahly Februari 23 itakayopigwa Uwanja wa Mkapa," alisema.

Katika hatua nyingine, tangu akiwa nchini Ethiopia, Manara kuwatangazia mashabiki kutojitokeza kuipokea timu hiyo hadi itakapofanya makubwa zaidi kwenye michuano hiyo, jana walijitokeza kwa wingi Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kuipokea timu hiyo huku pongezi kubwa wakizimimina kwa Kocha Mkuu, Mfaransa Didier Gomes, kwa ushindi huo.

## KAZE: UBINGWA YANGA BADO UPO

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze amesema kuwa malengo ya kuupata ubingwa msimu huu hayajapotea, bado yapo pale pale.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyoifanya idondoshe pointi mbili, Kaze alisema kuwa matokeo hayo ya sare hayawakatishi tamaa, badala yake yanawaongezea nguvu ya kupambana kwa ajili ya mechi zijazo.

"Malengo hayajapotea na sare hii haitotukatisha tamaa, kwa sababu naona kuna watu wanataka kutukatisha tamaa nia yetu ni kuupata ubingwa msimu huu," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema kuwa kipindi cha kwanza walitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hawakuzitumia, hiyo ilisababisha Mbeya City kuwa mchezoni kwa muda mrefu, lakini kipindi cha pili walipofanikiwa kupata bao ndipo ulipotokea uamuzi ambao alisema hapendi kuuelezea zaidi.

"Sitosema kilichotokea, lakini huwezi kuwa na ligi nzuri kama waamuzi watakuwa hivi, ila tu cha kusema tunajiandaa na mechi zinazofuata," alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mganda, Mathis Lule, yeye alisema kuwa aliisoma vizuri Yanga na kujua nguvu yao na udhaifu wao.

"Pointi moja ni muhimu kwa timu kubwa kama Yanga. Tulitaka tatu, lakini tumeipata moja. Haya yote yametokana na maandalizi. Tuliiangalia Yanga, wanatoka vipi nyuma, kati wanacheza vipi na mbele kwa hiyo tukapanga mikakati. Mwanzoni kuna wachezaji wetu hawakutekeleza majukumu vizuri, lakini baadaye walirekebisha makosa," alisema kocha huyo.

Kwa matokeo hayo, Yanga bado ipo kileleni ikiwa imefikisha pointi 45 kwa mechi 19 ilizocheza, huku Mbeya City ikishika nafasi ya 17, ikiwa na pointi 15 kwa idadi kama hiyo ya michezo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002